# Nipashe

Jumanne Machi 2, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580507

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


**Watano** wauawa kwa tuhuma za ujambazi Dar

UKURASA 3



**Mabadiliko** ya vigogo hospitali za rufani yaja

UKURASA 4


Nipashe TESA
Jumanne Machi 2, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Ripoti tabianchi ilivyoibua kitisho kikubwa kwa dunia
Jukumu kukiinua Kiswahili sasa lisiwe 'vita' bali elimu
Walio sokoni, mikusanyiko sasa anzeni kuvaa barakoa
ELIMU
NA MARCO MADUHU, SHINYANGA
'Nyumba za taka' zilipogeuka adui mkubwa makazi ya watu
• Vyanzo maradhi, wadudu, majitaka

UKURASA 11

# Adha inayowakumba wasafiri Mbezi Luis

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**JIJI LASALIMISHA GARI LA KIFAHARI SERIKALINI**

AGIZO la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, la kutaka wakurugenzi wa halmashauri nne nchini...

UKURASA WA 5

**WAKUMBWA HOFU VIFO SANGARA ZIWA VICTORIA**

BAADHI ya wakazi wa Manispaa ya Bukoba, mkoani Kagera wame-kumbwa na hofu baada ya...




Mamalishe wakiendelea na kazi zao katika eneo la kituo cha Magufuli Mbezi Luis Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana, wakisubiri kupangiwa eneo maalum la kufanyia biashara yao. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Serikali yaja na hatua uvamizi wa nzige

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play | Download on the App Store




## Mrithi wa Maalim Seif serikalini apatikana

UKURASA 2


MICHEZO **ONYANGO ATANGAZA KUJA KIZEE SIMBA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Uzalishaji Kiwanda cha mabomba cha Simba Pipe Industries, Jitin Pratap, namna kinavyotengeneza na kuzalisha mabomba ya maji yenye ubora na viwango stahiki katika ziara yake ya kujionea uzalishaji wa malighafi za maji jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Adha inayowakumba wasafiri kituo Mbezi Luis

**Na Mwandishi Wetu**

KUKOSEKANA kwa utaratibu na mpangilio wa wafanyabiashara wadogo katika kituo kikuu cha mabasi cha Magufuli, Mbezi Luis, mkoani Dar es Salaam, kumesababisha kero kwa abiria, magari na kupoteza mwonekano mzuri wa kituo hicho.

Baadhi ya mamalishe wameonekana wakifanya biashara ya kuuza chakula huku wakiwa na majiko yenye moto, hali inayohatarisha usalama wa abiria na magari.

Mwandishi wa gazeti alishuhudia majira ya asubuhi wafanyabiashara hao wakiwa wamezagaa kila eneo bila kuwa na utaratibu mzuri wa mabasi kuingia kituoni hapo.

Utaratibu uliopo sasa mabasi yanakoingilia ndiko kwenye maegesho ya bajaj, pikipiki na magari binafsi, jambo linalosababisha adha kubwa kwa abiria.

"Kituo hiki ni kizuri sana cha kimataifa, lakini kukosekana kwa utaratibu maalum wa kufanya biashara humu kunakichafua na kuonekana cha ovyo, ona wafanyabiashara wako kila mahali na wengine wana majiko ya kupikia hii ni hatari sana," alisema mmoja wa abiria, Monica John.

"Ona mama na baba ntilie wanauza chakula kila mahali, wengine wana majiko ya mkaa na kuni, na anakaa pembeni ya magari, inapoteza mwonekano, kama wanataka watu hawa wawepo kituoni ni muhimu kuwe na utaratibu mzuri ili kuwa na mwonekano mzuri na usalama," alisema.

Kadhalika, kwa sasa magari yanayotoka mikoa ya Kusini yanapoingia Dar es Salaam, hayaruhusiwi kushusha abiria njiani mpaka kituo cha Mbagala na Temeke na kituo cha mwisho ni cha Mbezi.

Akizungumza na Nipashe kondakta wa moja ya gari linalofanya safari zake Kusini mwa Tanzania, alisema "Haturuhusiwi kushusha abiria zaidi ya vituo viwili yaani Temeke na Ubungo (kwa sasa Mbezi Mwisho), tukishusha njiani tunakamatwa."

Mmoja wa abiria aliyekuwa ndani ya gari hilo aliyekuwa anashukia kituo cha Tabata Matumbi, Rosemary Joseph, alisema kumpeleka Mbezi mtu anayeshuka Tabata ni kumpotezea muda na kumsababishia gharama.

Abiria hao walishauri ni vyema serikali ikaweka utaratibu wa mabasi ya mikoa ya Kusini ambayo hupita Barabara ya Kilwa na yanayopita Barabara ya Bagamoyo kushusha abiria njiani, badala ya mpaka kupelekwa Mbezi.

Aidha, watumiaji wa kituo hicho waliomba uwekwe utaratibu maalum wa kuingia na kutoka kituoni humo ili kuondoa kero ya foleni katika makutano ya barabara hiyo ambayo kwa sasa hakuna taa.

"Kwenye makutano ya barabara ya Morogoro magari yanayotoka Ubungo yanayoelekea kituoni yanatakiwa kuzunguka kando kidogo ya barabara kuu na kuingia upande wa pili, huku yanayotoka Chalinze yanatakiwa kuzunguka ndiyo yaingie kituoni humo, bila kuweka utaratibu eneo hili limegeuka kuwa kero kubwa nyakati za asubuhi na jioni," alisema mmoja wa abiria.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa Kituo cha Mabasi cha Magufuli, Maira Chilosa, alisema jana imefanyika operesheni ya kuondoa mamalishe waliokuwa na majiko ndani ya kituo na kuweka eneo maalum wakati wanasubiri ujenzi wa eneo la kupikia.

"Eneo lao (mamalishe na babalishe) limefanyiwa upembuzi yakinifu na baada ya kukamilika watakuwa na eneo la kupikia, kwa sasa tumewaondoa ndani ya kituo kwa kuwa ni hatari kwa magari na watu, anaruhusiwa kuuza vitu vilivyopikwa, vikavu na bidhaa nyingine na siyo kupikia ndani ya kituo," alifafanua.

Alisema kituo hicho kinasimamia utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli kuwa wafanyabiashara wadogo waruhusiwe na kwamba utaratibu unafanyika ili kutowasumbua, lakini kuwe na utaratibu wa kutunza kituo hicho.

Kuhusu waendesha bodaboda na pikipiki, alisema wamepokea malalamiko ya kuongezeka kwa madereva wa vyombo hivyo huku wenyeji waliowakuta wakishindwa kufanyabiashara na kwamba jitihada za kuwaandalia eneo maalum unaendelea.

Kuhusu wapigadebe, alisema watu 48 wamekamatwa jana na kupandishwa mahakamani kwa kosa la kubugudhi abiria na kupigwa marufuku kupiga debe ndani na nje ya kituo hicho.

Akizungumzia mabasi yanayofanya safari mikoani, alisema magari yote yanatakiwa kuanzia ndani ya kituoni hicho na walifungua ofisi za kupakia na kushusha abiria maeneo ya Shekilango hawaruhusiwi kufanya hivyo na watakaokaidi watachukuliwa hatua.

Nipashe iliwatafuta wasemaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), ambao walisema wana vikao vingi huku Mkurugenzi wa Udhibiti wa Huduma za Barabara, Johansen Kahatano, simu yake ikiita bila kupokewa.

# Othman Masoud amrithi Maalim Seif

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amemteua Othman Masoud Othman Sharif, kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar.

Katika taarifa ya vyombo vya habari iliyotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Zena Ahmed Said, ilisema kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 9(3) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kinachosema kwamba "Muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utakuwa wa Umoja wa Kitaifa na utendaji wa kazi zake utafanywa katika utaratibu utakaohakikisha kuendelezwa kwa umoja nchini na lengo la kufikia demokrasia." Othman anachukua nafasi ya Maalim Seif Sharif Hamad aliyefariki dunia Februari 17, mwaka huu.

Kwa mujibu wa uwezo aliopewa chini ya kifungu namba 39(3) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, baada ya kushauriana na Chama cha ACT-Wazalendo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Mwinyi amemteua Othman Masoud Sharif kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Sharif alikuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa awamu ya kwanza ya Rais Dk. Ali Mohamed Shein.

Sherehe ya kuapishwa kwa Makamu huyo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar zitafanyika leo Machi 2, 2021 saa 4:00 asubuhi katika ukumbi wa Ikulu, Zanzibar. Kabla ya uteuzi mpya Othman alikuwa mshauri wa masuala mbalimbali kutoka katika Chama cha CUF na baadaye alipohamia ACT-Wazalendo ikiwamo sheria baada ya uteuzi wake wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ulipotenguliwa na Rais mstaafu Dk. Shein mwaka 2014. Othman ni msomi wa masuala ya sheria katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo kikuu cha Turin nchini Italia.

Ni mwanzilishi wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar (DPP), kufuatia maridhiano ya kisiasa ya muafaka katika kipindi cha Rais mstaafu Amani Abeid Karume na kuendelea na nafasi hiyo katika kipindi cha Rais mstaafu Dk. Shein na kupanda hadi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mapema mwaka 2010.

Uteuzi wa Othman ulitenguliwa mwaka 2014 baada ya kupinga rasimu iliyopendekezwa na Bunge la Katiba.

**APONGEZWA**

Baadhi ya viongozi wakiwamo wanasiasa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepongeza uteuzi huo na kusema ni sahihi kutokana na uwezo wake mkubwa katika masuala ya sheria na uongozi.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, Kheri James, alisema wanapongeza uteuzi huo na wapo tayari kumpa ushirikiano ili kutekeleza majukumu yake na kuendeleza maridhiano ya kisiasa Zanzibar.

Alisema hawana mashaka kuwa atakuwa msaada kwa Rais Dk. Mwinyi, Wazanzibari wote na atamuezi Maalim Seif Sharif Hamad kama kiongozi alieweka umoja na mshikamano. Aliwataka vijana wote kushirikiana katika kujenga umoja na mshikamano ili kuchochea shughuli za maeneo na uzalishaji mali, kujenga taswira ya amani, usalama na kivutio cha kweli cha nchi na kuwapa kichocheo cha fikra utendaji bora watendaji wa serikali katika kusimamia malengo yao.

"Kuendelea kuenzi umoja na mshikamano kama silaha ya mwanzo ya kuleta maendeleo kwa wananchi na taifa letu," alisema.

Alisema vijana wa Chama Cha Mapinduzi lazima wawe na dira ya kusisitiza, kuhimiza, kushikilia na kusimamia misingi ya umoja na mshikamano katika kusimamia misingi ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha ADA-Tadea na mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Juma Ali Khatib, alisema anamfahamu vizuri Othman wakati walipokuwa pamoja katika Bunge la Katiba akionyesha umahiri mkubwa katika masuala ya sheria na katiba.

Kwa upande wake Jaji Mkuu wa Zanzibar, Othman Makungu ambaye kabla ya uteuzi huo alikuwa Mwanasheria Mkuu wa serikali katika kipindi cha Rais mstaafu Dk. Shein, alisema anamfahamu vizuri kwa sababu alimpokea katika taaluma ya sheria katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika miaka ya 1989. Makungu alisema Othman ameteuliwa katika wadhifa ambao anastahiki kwa sababu anakuwa mshauri mkuu wa rais kazi ambayo ameifanya kwa muda mrefu akiwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali hadi kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Sheria katika kipindi cha utawala wa Rais mstaafu Dk. Salmin Amour.

Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini kwa tiketi ya CCM, Machano Othman Said, alisema uwezo wa Othman unafahamika katika kipindi alichofanya kazi akiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali pia akiwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kusaidia marekebisho mengi ya kisheria.

"Mimi nimekuwa mwakilishi kwa muda wa miaka kumi na tano sasa nilikuwa naye Othman wakati huo akiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Baraza la Wawakilishi, uwezo wake ni mkubwa katika masuala ya sheria...matarajio yangu makubwa atasaidia na kufanya kazi vizuri na Rais Dk. Mwinyi," alisema Machano.

HABARI KITAIFA

## Watuhumiwa watano ujambazi wauawa

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limewaua watu watano wanaotuhumiwa kuwa ni majambazi na kukamata bastola aina ya STAR iliyofutwa namba ikiwa na risasi tatu ndani, kasha na maganda mawili ya risasi yaliyotumika.

Kamanda wa Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kwamba watu hao waliuawa Jumamosi saa 12:00 asubuhi maeneo ya Kivule kwa Iranga.

Alisema Jeshi la Polisi kupitia kikosi chake cha kupambana na ujambazi liliwaua watu hao waliokuwa kwenye gari namba T 836 DHF aina ya Toyota Noah.

"Majambazi wapatao sita wakiwa kwenye gari hilo wakiwa wanakwenda kufanya uhalifu maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, kabla hawajatimiza lengo lao, kikosi kazi cha Jeshi la Polisi kiliweka mtego na kufanikiwa kuzuia ujambazi huo kwa kutaka kuwakamata wahalifu hao, lakini majambazi hao walitoka kwenye gari na kuanza kukimbia huku wakiwarushia askari risasi na hatimaye askari walijibu mapigo na kuwapiga risasi watu watano ambao walifariki dunia papo hapo," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema mmoja kati ya watuhumiwa hao alifanikiwa kukimbia huku akifyatua risasi ovyo na kumjeruhi askari mmoja.

"Baada ya kuwapekua walikutwa na bastola moja ikiwa na risasi tatu ndani ya magazine na maganda mawili ya bastola. Miili ya marehemu imeifadhiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)," alisema.

Katika tukio lingine, kamanda alisema operesheni iliyofanyika siku mbili kuanzia Jumapili, kuwasaka wezi wa pikipiki imewakamata watu 10 na pikipiki 16.

Kamanda Mambosasa aliwataja baadhi yao waliokamatwa kuwa ni Stephen Paul (38), mkazi wa Ulongoni A, Salum Mustafa (28), mkazi wa Kigogo na Nsajigwa Kaisi (25), mkazi wa Mongo la Ndege A.

"Operesheni hii ilifanyika baada ya kupokea taarifa toka kwa walioibiwa pikipiki zao katika matukio haya ambayo yamekithiri maeneo mbalimbali Dar es Salaam," alisema.

Alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakiiba pikipiki katika maeneo mbalimbali Dar es Salaam na kuzipeleka kwa madalali ambao huziuza.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, akipokea hati za utambulisho kutoka kwa Kansela Mkuu wa China, Zhang Zhisheng. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kuchukua hatua uvamizi nzige

**Na Godfrey Mushi**, MOSHI

SERIKALI inafuatilia 'kusuasua' kwa Shirika la Nzige wa Jangwani kupambana na kundi jipya la nzige lililoingia nchini wilaya za Longido na Monduli mkoani Arusha, na kuahidi kuchukua hatua kama shirika hilo halitaongeza juhudi.

Jana, Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alisema amezungumza na Wizara ya Mambo ya Nje pamoja na Balozi wa Tanzania nchini Ethiopia, kuhusu suala hilo, kutokana na Tanzania kutoridhishwa na utendaji wa shirika hilo.

Mara ya kwanza nzige zaidi ya milioni 50 waliripotiwa kuingia nchini Februari 19, mwaka huu, kupitia Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro na baadaye kuelekea baadhi ya maeneo ya vijiji vya wilaya ya Same na Simanjiro, mkoani Manyara.

"Tumeongea na Wizara ya Mambo ya Nje, Balozi wetu kule Ethiopia atakuwa amemwita Mkuu wa shirika hili, kumweleza kwamba tungependa tuone kweli wako makini zaidi, na sisi ni wanachama na tumelipia fedha na Tanzania ni kati ya nchi mbili ambazo zimelipa ada yote ya uanachama. Ndege za shirika hili ni ndege zetu sisi wote, lakini hili shirika lina ndege iko Moshi, muda wote imetua wamemchukua rubani wamempeleka Kenya."

"Nimejaribu sana kumpigia simu, Mkuu wa shirika hili simpati, ameambiwa kwamba namtafuta na amepewa namba yangu hajanipigia simu. Kwa hiyo nampelekea tu salamu kwamba haturidhishwi na utendaji wake, sisi kama wanachama na inawezekana kama uzembe ni wa kiasi hiki ambacho nimeuona, si ajabu kwamba tukaona hii shughuli ya kupambana na nzige wa jangwani, bado inaendelea kuwa changamoto.

"Kwa hiyo tunataka tuone hili shirika likifanya kazi vizuri, tumetoa pesa zetu za Watanzania na tunajua wanapata misaada kutoka mashirika mbalimbali, waongeze juhudi. Haiingii akilini kwa nini kuna ndege iko Moshi imetua muda wote bila kumwaga viuatilifu, lakini hairuki kwa sababu wao wamemchukua rubani aliyekuwa hapa na wamempeleka Kenya."

Prof. Mkenda alisisitiza: "Kwa hiyo tutaendelea kulifuatilia hili na tutachukua hatua madhubuti kama uongozi wa shirika hili hautaongeze juhudi za kupambana na nzige. Lakini kwa ujumla napenda kuwahakikishia Watanzania kwamba tuko makini sana na tunatumia capability zote (nguvu), kuwamaliza nzige hawa na mpaka sasa hivi hatujapata madhara ya aina yoyote kutokana na nzige walioingia hapa Tanzania."

Kwa mujibu wa Waziri Mkenda, sasa hivi kuna kundi jipya limeingia kutoka Kenya ambalo lipo Longido.

"Kwa Wilaya ya Siha (Kilimanjaro), tumewateketeza wale ambao walikuwa wameingia, lakini kakundi kadogo kaliescape (kalikimbia) kakarudi Longido, baada ya kukaa na kufuatiliwa, wakaruka wameenda Monduli. Kundi hilo sasa hivi wataalamu wako pale wanalifuatilia kwa ajili ya kuliangamiza.

"Kuna kundi jipya la nzige wachanga sana limeingia kutoka Kenya, limeingia Longido na sasa hivi tunajua mahali lilipo, tunasubiri kwenda kuliteketeza. Tuna helikopta inaweza ikaondoka muda wowote kutokea Uwanja wa Ndege wa Arusha, kwa ajili ya kwenda kumwaga viuatilifu pale na itaenda tena Wilaya ya Monduli.

Prof. Mkenda alisema nzige wengi wamekufa baada ya kunyunyuziwa dawa aina ya Fenitrothion 96% ULV, kwenye maeneo ya mapori na nzige hao walitua makundi kwa makundi.

Vile vile, amesema kuna kundi moja liko Simanjiro ambalo wanaendelea kuliteketeza, lakini kwa sababu ya mazingira ya Simanjiro, wamepata shida kwa sababu limeingia maeneo yenye miiba na vichaka vikubwa, na wataalamu waliopo huko wanashindwa kulielewa sasa hivi liko wapi.

Waziri Mkenda, amedai kuwa kuna dalili kwamba huenda likawa limevuka kwenda Wilaya ya Kiteto au bado liko Wilaya ya Simanjiro.

**WAOMBA NDEGE TANAPA**

Wakati vita dhidi ya nzige hao wa jangwani ikiwa imeshika kasi, Waziri Mkenda, alisema tayari wizara yake imeomba ndege ndogo ya ufuatiliaji ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kusaidia kwenda kuangalia angani kundi hilo ili baadaye helikopta iende ikawapige sumu nzige hao mahali popote walipo.

"Tumeongea vile vile na Wizara ya Maliasili na Utalii, kuwaomba kwamba zile Hifadhi za Taifa zote pamoja na misitu ya serikali ambayo iko mpakani, wafanyakazi waliopo kule na wenyewe wawe macho, waangalie kama kuna kundi lolote litakuwa linaingia na maeneo ambayo hakuna wananchi ambao wanatupa taarifa, basi watupe taarifa tuende tukapambane nao.

"Ndege ya Survilance ya TANAPA (ndege ya ufuatiliaji), haiwezi kunyunyuzia, lakini itakuwa inaongeza nguvu, kwa ajili ya kuruka kuangalia maendeleo yanavyoenda."

**HELIKOPTA YA NZIGE WEKUNDU**

Waziri Mkenda alisema pia serikali imeleta helikopta kutoka Shirika la Kupambana na Ndege Wekundu nchini Zambia.

Alisema kwa kuwa ndege hiyo ni wanachama wote wa shirika hilo na tayari imeshaondoka Zambia na imeshatua nchini. Jana (juzi) ilikuwa inafanya ufuatiliaji na leo (jana) ilikuwa inanyunyiza sumu katika maeneo ya Longido na Monduli.

"Tunaendelea kufuatilia nini kinaendelea katika mwenendo wa nzige, tunafuatilia sana juhudi za Kenya za kupambana na nzige hawa na tunawasiliana nao. Nafurahi kusema kwamba hata kuna kundi moja lilikuwa linavuka mpaka, lakini lilishambuliwa na Kenya na kuteketezwa.

Wenzetu nao kule (Kenya) wamerusha ndege kuhakikisha kwamba wanaua nzige hawa kama ambavyo sisi tunafanya upande huu," alisema.

**UPEPO MBAYA**

Alisema wamepata taarifa kwamba kuna kundi jingine linakuja kutokea Machakos, hivyo upepo unaweza ukawa unawaleta kupitia upande wa Kajiado kuja Tanzania.

Prof. Mkenda alisema kuwa tayari wameshawasiliana na Kenya, wakitaka kuliwahi kundi hilo kuliangamiza.

"Tunajua nzige hawa wanasafiri kilomita 80 kwa siku na wakishafika wanatua. Mara nyingi tunawashambulia wakiwa chini, kwa jioni wanatua wanalala, asubuhi kwa ndege unaweza ukawapiga au ukawahi ukawapiga jioni.

Hizi ndege ni ndogo na wakati mwingine hatuzitumii kumwaga sumu jioni, kwa sababu haziruki kwenye giza, ndio maana jioni tunawatumia wanaokuwa na pampu za mkono.

Hizi juhudi tunazofanya sasa hivi mtashangaa kwa nini tumechukua ndege helikopta kutoka Shirika la Kupambana na Nzige Wekundu lenye makao makuu yake Zambia, ambalo sisi ni wanachama na tunalipia, wakati nzige hawa sio nzige wekundu, hawa ni nzige wa jangwani na sisi vile vile ni wanachama wa Shirika la Kupambana na Nzige wa Jangwani, lenye makao makuu Ethiopia."

HABARI KITAIFA

# Wakurugenzi wanaorudisha fedha Hazina waonywa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amewaonya Wakurugenzi wa Halmashauri nchini kuacha tabia ya kurudisha fedha za maendeleo Hazina kwa kutotumika kama ilivyokusudiwa baada ya mwaka wa fedha kuisha.

Kufuatia hali hiyo, amewaagiza kuhakikisha fedha zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa miradi hiyo kwa mwaka 2020/21, zinatumika kama ilivyokusudiwa kabla ya Mei 30, mwaka huu.

Vilevile, amesema leo atatoa taarifa maalum ya utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kuhusu ujenzi wa vyumba vya madarasa ambalo mwisho wake ulikuwa Februari 28, mwaka huu.

Waziri Jafo aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Alifafanua kuwa katika robo ya pili na ya tatu ya mwaka wa fedha 2020/21, halmashauri zimeshapokea fedha za miradi ya maendeleo wastani wa Sh. bilioni 245.29 sawa na asilimia 38.99 ya bajeti iliyokuwa imetengwa.

"Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioisha kuna baadhi ya halmashauri zilipokea fedha ya afya, ambayo kwa bahati mbaya sana fedha nyingi zilirudi Hazina bila kukamilisha miradi kwa sababu mwaka wa fedha ulikuwa umeisha," alisema.

Aliongeza: "Kwa mwaka huu hatutarajii kuona halmashauri yoyote iliyopokea fedha kurudisha Hazina kutokana na kutotumika. Hatutaki kuona inapofika Juni 30, mwaka huu, fedha inarudi Hazina."

Waziri Jafo alisema itakapofika Mei 30, mwaka huu, ujenzi wa wodi, zahanati, madarasa na miundombinu mingine uwe umekamilika.

"Hatutamwelewa Mkurugenzi yeyote katika mwaka huu wa fedha, kwamba fedha zimerudi Hazina ilhali bado wananchi wanataabika katika ujenzi wa miundombinu kwenye maeneo yao," alisema.

Aliwataka wakurugenzi ambao wamepokea fedha kabla ya Mei 30, mwaka huu, miundombinu yote iwe imekamilika.

"Kwa mwaka wa fedha 2020/21 bajeti iliyokuwa imetengwa ya miradi ya maendeleo ya Sh. bilioni 629.1 ambayo tayari halmashauri zimepokea Sh. bilioni 245.29, naomba niwaambie tutakuwa site kufuatilia utekelezaji wa maagizo haya," alisema.

Alibainisha kuwa fedha hizo ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo ikiwamo ujenzi wa majengo ya utawala ya halmashauri, wodi tatu katika hospitali 67 ambazo ziliongezeka.

# Mabadiliko ya uongozi hospitali za rufani yaja

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ameagiza kufanyike kwa mabadiliko ya uongozi wa timu za uendeshaji wa hospitali zote 28 za rufani za mikoa kulingana na nafasi ya kila kiongozi alivyoshiriki kusababisha hasara kuanzia kwa mganga mfawidhi wa hospitali.

Waziri aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari, na kueleza kuwa amekuwa akipokea malalamiko mengi toka kwa wananchi kuhusu kukosekana kwa dawa na vipimo katika vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi zote kinyume cha matarajio.

Alisema ili ukweli ujulikane na haki itendeke, wizara iliunda kamati ya wataalamu kutoka wizara na taasisi za sekta mbalimbali ili kufuatilia hospitali za rufani 28 za mikoa kwa kipindi cha miezi 18 kuanzia Julai 2019 hadi Desemba 2020. "Lengo lilikuwa ni kubaini changamoto zinazochangia upatikanaji duni wa dawa na vipimo licha ya kuongezeka kwa mtaji wa dawa," alisema.

Waziri alisema jumla ya bidhaa za dawa na vipimo 25-30 kati ya nyingi zilizopo kwenye orodha ya bidhaa za afya kwa kituo husika zilifanyiwa ufuatiliaji kuanzia ununuzi, mapokezi na matumizi.

Alisema amepokea taarifa ambayo imethibitisha uwapo wa uzembe na kutojali katika usimamizi wa mfumo wa ugavi wa bidhaa za afya, viashiria vya hujuma, wizi na udokozi wa bidhaa hizi. Alisema upungufu huo unachangiwa na utendaji wa mazoea wa baadhi ya viongozi wasio waadilifu na wasiowajibika katika kusimamia rasilimali kuanzia ngazi ya taifa, mkoa, Halmashauri pamoja na watumishi mmoja mmoja katika maeneo yao ya kazi.

"Jumla ya thamani ya fedha ambazo imethaminishwa kwa mapungufu haya inakadiriwa kuwa siyo chini ya Sh. bilioni 26.7 kwa kipindi hiki kifupi kwa bidhaa hizo chache.

Alisema kwa mujibu wa matokeo ni dhahiri kuwa na usimamizi dhaifu wa mifumo ya udhibiti wa mali ya umma, dalili za hujuma, wizi na uwajibikaji usiofaa wa bidhaa hizi za viongozi katika ngazi zote za uongozi hadi kwa mtumishi mmoja mmoja.

"Sababu hizi ni mojawapo ya mambo yanayosababisha kukosekana kwa bidhaa za afya au kutotosha na mtaji kudidimia. Kufuatia hali hii Februari 28, mwaka huu, niliitisha kikao na waganga wakuu wa mikoa yote, waganga wafadhili wa hospitali zote za rufani za mikoa pamoja na menejementi ya wizara wakiwamo wawakilishi kutoka Ofisi ya Rais (TAMISEMI) niliwaeleza matokeo ya taarifa ya ufuatiliaji uliofanyika," alisema.

Alisema baada ya kuwaeleza aliwasikiliza na wengi wao walikiri upungufu uliobainishwa na kamati.

Waziri alisema kutokana na hali hiyo amemwagiza Katibu Mkuu wa afya kuchukua hatua za nidhamu kwa kila mtumishi ama mtu yeyote aliyekwenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za ununuzi na ugavi wa bidhaa za afya.

"Aunde kamati kwa kushirikiana na ofisi ya Rais ya TAMISEMI kufanya mapitio ya mikataba ya washiriki wa bidhaa za afya nchi nzima na kushauri ipasavyo juu ya hatua stahiki za kuchukua," alisema.

Waziri alisema kuratibu zoezi la maboresho ya miongozo ya ushiriki na ofisi ya TAMISEMI na makatibu tawala wa mikoa kwenye kuimarisha ufuatiliaji na uangalizi wa uendeshaji wa hospitali hizo.

Aidha, ameagiza ndani ya siku 14 kuanzia jana Katibu Mkuu kumpatia taarifa ya utekelezaji inayojibu masuala yote yaliyoibuliwa kwa kuwa yametokea wakati halmashauri na mikoa wapo waganga wakuu wa halmashauri na mikoa husika wanaowakilisha wizara katika kusimamia huduma za afya.

"Vilevile hapa wizarani wapo wataalamu wabobezi ikiwamo kurugenzi zinazohusika na usimamizi na ufuatiliaji wa uendeshaji wa hospitali hizo hususani idara ya tiba na huduma za uchunguzi pamoja na idara ya mfamasia mkuu wa serikali," alisema.




Ofisa wa Wakala wa Vipimo (WMA), Glory Mtana, akitoa elimu kwa watu waliofika kwenye banda hilo, kuhusu umuhimu wa kuzingatia vipimo sahihi wakati wa wiki ya viwanda kwa wanawake na maonyesho ya bidhaa mbalimbali jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jiji lasalimisha gari la kifahari serikalini

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

AGIZO la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, la kutaka wakurugenzi wa halmashauri nne nchini kujieleza kwa nini walinunua magari ya kifahari, limezaa matunda baada ya Jiji la Mwanza kusalimisha serikalini gari lililonunuliwa kwa ajili ya mkurugenzi wake.Majaliwa akiwa katika ziara ya siku mbili mkoani Mwanza, mwezi Desemba mwaka jana, alitoa siku saba kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, maofisa wanaochambua maombi ya ununuzi wa magari katika Ofisi ya Waziri Mkuu na wakurugenzi wa Jiji la Mwanza, Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Msalala na Kahama wajieleze kwa sababu gani magari hayo yalinunuliwa kwa gharama kubwa. Akizungumza na Nipashe jana, Meya wa jiji hilo, Sima Sima, alisema tayari wametekeleza agizo hilo na kwamba wamefuata maagizo ya Waziri Mkuu la kufuata taratibu za ununuzi wa magari zilizotolewa na serikali.

Alisema kuna mwongozo wa serikali ambao unaainisha gharama pamoja na aina ya gari kwa ajili ya mkurugenzi, meya wa jiji pamoja na wakuu wa idara.

Alisema taratibu hizo zilipaswa kufuatwa na kwamba mali walizopaswa kurudisha serikalini tayari zimerudishwa.

"Jiji la Mwanza tumetekeleza agizo la Waziri Mkuu, lakini tumeendelea kufuata taratibu za ununuzi wa magari kwa kufuata waraka ambao umetolewa na serikali wa aina ya magari ambayo tunapaswa kununua na baadhi ya mali zilizopaswa kurudishwa tumeishazirudisha na sasa hivi tupo mchakato wa kununua magari ambayo yanastahili halmashauri zetu," alisema.

HABARI KITAIFA

## Mwalimu kuishtaki CWT madai ya kashfa

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MWALIMU wa Shule ya Msingi Kipande, wilayani Nkasi mkoani Rukwa, Selis Ndasi, anakusudia kukifikisha mahakamani Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na kudai fidia ya Sh. milioni 100 kwa madai ya viongozi wa chama hicho kumkashifu na kuondolewa katika nafasi yake ya uenyekiti wa CWT Wilaya ya Nkasi kinyume na katiba ya chama.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Ndasi alisema kupitia wanasheria wake ametoa notisi ya siku 14 akielezea kusudio lake la kukifikisha mahakamani chama hicho kutokana na ukiukwaji wa katiba na kumkashifu.

"Barua ya kunisimamisha uenyekiti wa wilaya wa CWT ya Oktoba 7, 2019 wameeleza sababu ni kwamba eti nilikosa uadilifu… lakini Katiba ya CWT inafafanua kukosa uadilifu ni kutumia mali za chama vibaya na kufanya ubadhirifu wa fedha za chama…sasa nataka wakanieleze ni ubadhirifu upi au mali nilizoharibu hadi kunisimamisha uongozi," alisema Ndasi.

Alisema; "Kwa mujibu wa Katiba ya CWT ibara ya 15.2, ibara ndogo (I) inaeleza kuwa kumsimamisha uongozi kiongozi wa kuchaguliwa atakayebainika kukiuka taratibu za chama au kufanya ubadhirifu wa mali na fedha za chama katika ngazi ya wilaya atapelekwa katika mkutano mkuu wa wilaya kwa hatua zaidi kitu ambacho hakikufanyika."

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, akihojiwa kwa njia ya simu alikiri kupokea notisi ya kusudio la kufikishwa mahakamani na mwalimu huyo na kudai amewasilisha idara ya kisheria ya CWT ambako wanaichakata na kwamba hawezi kuzungumzia zaidi suala hilo.

# Wakumbwa hofu vifo vya sangara Ziwa Victoria

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

BAADHI ya wakazi wa Manispaa ya Bukoba, mkoani Kagera wamekumbwa na hofu baada ya kuonekana samaki wengi kufa na kuelea katika Ziwa Victoria.

Wakizungumza na Nipashe, wakazi hao walisema kuwa kila mwaka kati ya mwezi Januari na Februari, huonekana samaki aina ya sangara waliokufa wakielea ziwani ambao huokotwa na kutumiwa kama kitoweo maarufu kama 'kifelezi'.

"Kwa kawaida huwa wanakuwa hawajaharibika, wa sasa wameharibika kiasi kwamba hawawezi kuliwa, tumezoea kila mwaka huwa tunawaokota wakiwa wamekufa juu ya maji, lakini hatujafahamu kwanini hawa wameharibika," alisema Sadick Omary mkazi wa Nyamkazi.

Baadhi ya wavuvi waliozungumzia suala hilo akiwamo Richard Gasper, walisema kila siku wanakwenda ziwani kuokota samaki hao na kuwauza na kudai kuwa uwapo wa kitoweo hicho ni neema kwao.

"Hata mimi nimetoka kuokota leo, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema hii maana tunapata kipato kama laki moja ama laki moja na elfu ishirini maisha yanasonga, na ni kila mwaka sio mwaka huu tu," alisema Gasper ambaye mbali na kuwa mvuvi ni diwani wa kata Miembeni. Ofisa Uvuvi Mkoa wa Kagera, Ephrazi Mkama, alisema kuna sababu mbalimbali zinazoweza kusababisha samaki hao kufa ikiwamo ya kiasili ambayo husababisha mabadiliko ya tabia nchi na kubadilisha hali ya hewa ziwani. "Hali ya hewa inapobadilisha inaweza kusababisha ongezeko la virutubisho ambavyo husababisha baadhi ya magugu maji na wadudu maji kuongezeka ziwani, vyote hivi kutegemea hewa ya Oksijeni (Oxygen) ndani ya maji na kusababisha matumizi ya hewa hiyo kuwa makubwa," alisema Mkama.

Alisema kuwa hewa hiyo hupenya na kuingia ndani ya maji na sehemu yenye kina kirefu cha maji inakuwa na Oksijeni kidogo ikilinganishwa na sehemu ya juu, na kwamba joto lipoongezeka husababisha upungufu wa hewa hiyo, hivyo samaki anayetegemea kuishi kwa kutegemea hewa hiyo, inapopungua hupata madhara na wakati mwingine hufa.

"Sababu nyingine inayoweza kusababisha vifo vya samaki ni uwepo wa wadudu maji ambao baadhi yao husababisha sumu ndani ya maji, kwa sababu samaki anakula wadudu hao kama chakula hasa sangara ambaye pia hula samaki wenzake, husababisha kiwango cha sumu kinachotokana na bakteria hao kuongezeka na kuathiri mfumo wa hewa na moyo wa samaki," alisema.

Aliwataka wananchi wanapoona samaki waliokufa wakielea, wachukue tahadhari na kutowatumia kama kitoweo ili kuepuka kupata madhara endapo watakuwa wamekufa kutokana na kula chakula chenye sumu inayotokana na wadudu maji au inayotengenezwa na binadamu.

"Kuna majani wananchi wanayachukua na kuyapondaponda kwa ajili ya kuyatumia kuvuna samaki ziwani, sumu hizi zina madhara kwa samaki kufa, lakini kwa binadamu atakayekwenda kumtumia huyo samaki kama kitoweo," alisema.

Naye mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) kituo cha Nyegezi mkoani Mwanza, Enock Mlaponi, alisema wamekwishachukua sampuli na kuipeleka kwa Mkemia Mkuu ili kuona kama samaki hao wana madhara kwa binadamu na wanachosubiri ni majibu.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohammed, akimkabidhi mmoja wa madereva wa magari ya usafi ufunguo wa moja kati ya magari manne ya kubebea taka yaliyotolewa na Shirika la Misaada la Romania (RoAID), kwa manispaa za mkoa wa Mjini Magharibi na Baraza la Mji Chakechake. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# USAID yawekeza Dola mil. 48 uhifadhi mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), imewekeza Dola za Kimarekani milioni 48 katika uhifadhi wa mazingira.

Taarifa ya Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Dk. Donald Wright, ilisema jana wakati wa maadhimisho ya miaka mitano ya mradi wa kuhifadhi mifumo ya ikolojia iliyo hatarini Kaskazini mwa Tanzania (EENT) kwa kulinda nyanda za malisho zenye afya zilizounganisha maeneo yote ya ikolojia ya Tarangire/ Maasai Kaskazini mwa Tanzania.

Alisema USAID EENT, mradi wa miaka mitano wa Dola za Kimarekani milioni 10.1, ulibuniwa kulinda shoroba muhimu za Kaskazini mwa Tanzania, ambazo zina ukubwa wa takribani ekari milioni 8.6, zinazounganisha mfumo wa ikolojia wa Serengeti Magharibi na ikolojia ya Amboseli Mashariki.

Balozi Wright alisema mfumo huo wa ikolojia ni maarufu kwa uhamaji wa mamalia na ni wa tatu kwa ukubwa duniani ndani ya Afrika Mashariki (baada ya Serengeti na Sudani Kusini), nyumbu, pundamilia na wanyamapori wengine huhama kwa msimu kupata chakula na maji.

"Mradi umechangia katika afya na muunganiko wa ikolojia hii kwa kiwango kinacholingana na vitisho vya sasa vya mabadiliko ya tabia nchi na mahitaji ya rasilimali. Kama matokeo ya utekelezaji wa mradi huo, zaidi ya Watanzania 47,000 wamepata faida kubwa za kiuchumi kutokana na usimamizi endelevu wa maliasili. Kwa kuongezea, taasisi 46 zimeboresha uwezo wao wa kutathmini au kushughulikia hatari za mabadiliko ya hali ya hewa," alisema. Alisema miaka mitano ya kuhifadhi mifumo ya kiikolojia iliyo hatarini Kaskazini mwa Tanzania, ambayo ilionyesha mafanikio ya mradi huo, pamoja na jinsi ulivyoboresha usimamizi wa maliasili kwa zaidi ya hekta milioni 2.1 za maeneo muhimu kibaiolojia.

"Kuimarisha muunganiko na uhai wa ikolojia wa nyanda za juu za kaskazini ni muhimu kusaidia wanyamapori na jamii za wafugaji Kaskazini mwa Tanzania wakati wa kukuza ustawi wa uchumi wa sekta za utalii na mifugo," alisema Balozi Wright. Akizungumza kwenye mkutano na waandishi wa habari uliofanyika kwa njia ya mtandao, Mkurugenzi Mkazi wa USAID, Andy Karas, alisema; "Maliasili ya Tanzania ndio msingi wa maendeleo ya nchi; robo tatu ya idadi ya watu wanategemea moja kwa moja ardhi kwa maisha yao. Rasilimali hizi, ambazo zinawezesha utalii wa wanyamapori husababisha ukuaji wa Pato la Taifa."

"Kwa kutambua kuwa sababu za umaskini na upoteaji wa baioanuai vina uhusiano wa moja kwa moja, USAID inashirikiana na serikali ya Tanzania kuboresha utawala bora na usimamizi katika ngazi za nyanda, ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa taifa kupunguza biashara haramu ya wanyamapori na ujangili."

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kero za usafiri Mbezi Luis zipate ufumbuzi

**KITUO** Kikuu cha Mabasi cha Magufuli kilichopo Mbezi Luis Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, kimeanza kazi, lakini kuna mambo ya msingi lazima yafanyiwe kazi ili kiendelee kuwa bora na safi muda wote.

Mathalani, baadhi ya mama na babalishe hawana maeneo ya kupikia, kiasi cha baadhi kuingia na majiko ya mkaa kituoni, jambo ambalo ni hatari. Tunashukuru mamlaka ya usimamizi imewaondoa na kuwapa eneo la muda la kupikia, huku wafanyabiashara wanaoruhusiwa kuingia kituoni wakiwa ni wanaouza bidhaa za vyakula vilivyopikwa na vingine ambavyo siyo hatari.

Kituo hicho ni kizuri na bora Tanzania kutokana na majengo ya kisasa na mpangilio mzuri uliopo, na kama kitasimamiwa kama inavyotakiwa, kitaendelea kuwa na maana ya uanzishwaji wake na kitahudumia abiria vizuri.

Kwa sasa bado hakuna mpangilio mzuri wa wasafiri na watumiaji wengine, namna ya kuingia na kutoka kiasi cha kutumia njia ya magari, huku kukiwa na ongezeko la bajaji na pikipiki ambazo hazina eneo maalum pa kuegesha.

Tangu kuanza kwa kituo hicho zimeibuka kero mbalimbali kama za wasafariri wa mikoa ya kusini kwamba wanaruhusiwa kushusha abiria kituo cha Mbagala na Temeke pekee, baada ya hapo kituo cha mwisho ni cha Magufuli.

Maana yake msafiri anayetakiwa kushuka Buguruni, Tabata au Ubungo hataruhusiwa kushuka njiani hadi mwisho au ashuke kabla na kutumia usafiri mwingine kwenda kwake.

Tunaona hakuna sababu ya kuzuia abiria kushuka njiani, bali kuwe na vituo maalum vya kushusha kwa kuwa kutaka kila abiria afike mwisho wa gari ni usumbufu na kuongeza msongamano eneo la kituo. Aidha, mabasi yanayotumia njia ya Bagamoyo yanashusha abiria njiani kwenye vituo vinavyoruhusiwa, lakini kwa njia mpya ya Goba ambayo inatumiwa na baadhi ya mabasi hawataweza kushusha jambo ambalo ni usumbufu kwa wasafiri.

Pia, kutokana na kuwapo kituo kipya magari yaliyokuwa na ofisi nje ya kituo cha Ubungo kama eneo la Shekilango hayataruhusiwa kutumia maeneo hayo bali yote kuanza na kumaliza safari zao ndani ya Kituo cha Magufuli.

Tunaona maamuzi hayo ni usumbufu mkubwa kwa wasafiri, mathalani baadhi ya mabasi yana ofisi Kigamboni ili kuwarahisishia abiria wameamua kusogeza huduma hiyo karibu kwamba basi lianzie kule likusanye abiria na kupita kituoni humo.

Kama suala ni kupata ushuru ungewekwa utaratibu mzuri wa kuhakikisha kila kampuni inalipa, na wakati huo inapunguza usumbufu kwa wasafiri kuhakikisha anapata huduma za usafiri kwa urahisi.

Tunaona hakuna sababu ya mtu anayekwenda Tabata kupelekwa hadi Mbezi na baadaye kurudi Tabata, kiuchumi anapoteza muda mwingi barabarani na unamlazimisha kutumia gharama kubwa ambayo ingeepukika kama angeshusha njiani.

Hakuna sababu ya mtu anayetakia kuteremka Ubungo au Mwenge kulazimishwa kuja hadi Mbezi, wakati inawezekama kabisa kumshusha eneo hilo na kumrahisishia.

Kituo kwenda Mbezi kisigeuke kuwa fimbo kwa wasafiri wanaotumia usafiri wa umma kwamba anatumia gharama kubwa kuliko nauli ya aendako, tunaona ni muhimu mamlaka husika zikaja na utaratibu mzuri wa kuhakikisha wasafiri hawasumbuki.

Kama ilivyofanyika kwenye miji mingine abiria wanapakiwa na kushushwa kwenye vituo maalum na siyo wote lazima wafike mwisho wa basi. Pia ni muhimu sana mamlaka za usimamizi zikasimamia kituo cha Magufuli ili kiendelee kuwa bora, kuruhusu shughuli za kipika na nyinginezo hatari ndani ya kituo mwisho wake ni janga kubwa kukinyemelea kituo hicho kilichojengwa kwa mabilioni ya fedha za walipakodi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# ‘Wamachinga’ waheshimu vituo vya mabasi, abiria

Na Christina Mwakangale

**UNAPOFIKA** kwenye vituo vya mabasi, madaraja na njia za wanaotembea kwa miguu utashawishika kusema taifa linahitaji uhamasishaji na elimu ya matumizi ya kila eneo na shughuli zake.

Ni kwa sababu kuna tatizo. Baadhi ya maeneo kama vituo vya daladala achilia mbali mabasi ya mikoani na nchi jirani kuvamiwa na wafanyabiashara ambao hufanya vile wanavyotaka. Sehemu za kupumzika abiria ili kujikinga jua na mvua wakati wakisubiri usafiri zimeathirika zaidi.

Pamoja na kwamba kujiajiri kwenye uchuuzi ni ajira inayotegemewa na Watanzania hasa vijana walio wengi, baadhi yao hufanya biashara vituoni na kugeuka kero kwa abiria.

Vituo hugeuzwa sehemu za kuuza maji, karanga, juisi, mihogo, mahindi ya kuchoma, mishikaki na vituo hivyo vinakuwa si mahali pa abiria pa kupumzikia bali jukwaa la biashara.

Kinachojiri si tatizo tu la mandhari, kero bali hata kubadili sura za miji kutokana na wafanyabiashara wadogo, kuchafua mazingira.

Dar es Salaam kila kuliko na vituo vya daladala hali ni hiyo. Iwe Makumbusho, Barabara za Mandela, Ali Hassan Mwinyi, Kilwa, Kawawa na Morogoro, wajasiriamali wamejikita.

Viti au sehemu za kukaa ni vichafu vina michirizi ya mafuta inayoweza kuchafua nguo za abiria, kutokana na upishi wa mihogo mshikaki, dagaa na pia vimejaa maganda ya miwa.

Kuna wakati abiria na wafanyabiashara hutupiana maneno ya kashfa kila mmoja akijetetea huku wasikilizaji na mashuhuda wakizipima hoja zao.

Abiria walisimama katika kituo cha daladala, ili kujikinga na jua kali la utosini lakini eneo la kupumzikia lina meza kubwa zilizopangwa matunda, juisi, maji, biskuti na pipi.

Muuzaji mmojawapo wa bidhaa hizo, anawataka abiria waliosimama mbele ya meza wasogee pembeni, kwa sababu wanawazuia wateja.

Kilichotokea ni mzozo mkali, abiria wakishikilia haki yao kwamba kituo ni maalum kwa ajili yao kupumzika na mfanyabiashara naye akidai anafanyabiashara popote.

Huu ni mfano ambao pengine upo katika maeneo tofauti, hususan miji mikubwa kama Mbeya, Mwanza, Arusha na Tanga, lakini zipo dalili kuwa wajasiriamali wanajipenyeza katika maeneo yasiyo rasmi kibiashara. Pamoja na ukweli kuwa biashara hufanyika kuliko na mkusanyiko mkubwa hasa katika vituo vya abiria, kuwapo na utaratibu ni lazima ili isiwe kero na ikiwezekana yatengenezwe maeneo maalumu kwa ajili yao.

Biashara itafanyika popote hata kama muuzaji akiwa pembeni ya kituo, si lazima kukaa ndani ya kituo na kuwanyima abiria maeneo ya kusubiri usafiri.

Wafanyabiashara hawa wanaamua kutumia njia za watembea kwa miguu zilizotengwa maalum, kwa kuweka meza zao za biashara au kupanga bidhaa zao za viatu, nguo kwenye vituo na kuwapa shida watembea kwa miguu.

Sehemu za barabara ambazo zimewekwa maalumu kwa watembea kwa miguu huko nako kuna bidhaa zimepangwa na kuwaacha wapambane na vyombo vya moto barabarani kutokana na maeneo ya kupita kuwa finyu.

Maeneo yaliyo na tatizo hili haya ni mojawapo, kituo cha Ilala Boma, Magomeni, Mlimani City, Makumbusho, Mombasa, Gongo la Mboto, Karume, Mbagala, Kariakoo na mengineyo, wafanyabiashara wamegeuza ni maeneo ya kazi, si kwa ajili ya kupumzikia abiria, kwa kuwa zimepangwa bidhaa.

Lilikuwa ni jambo rahisi kwa wafanyabiashara hizi, kwanza kwa kuhakikisha eneo analisafisha kila anapomaliza au kabla ya kuanza kufanya biashara yake.

Kituo cha abiria kinajaa maganda ya miwa hata kwa wiki nzima hayazolewi, chupa, mifuko, maganda ya mihogo, karatasi na vyote vinavyohusisha bidhaa zinazouzwa vituoni.

Wasimamizi wa maeneo haya zikiwamo, halmashauri, maofisa afya na madiwani wasimamie usafi na kutoa elimu ya utunzaji maeneo ya biashara na kuheshimu sehemu mbalimbali zilizotengwa kwa ajili ya kazi mbalimbali badala ya kuacha mambo kubaki ‘segemnege’.

HABARI KITAIFA

# Zitto: Maalim Seif aliwaandaa warithi

**Na Maulid Mmbaga**

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Hayati Maalim Seif Sharif Hamad, kabla ya kufikwa na umauti alishawaandaa watakaomrithi.

Maalim Seif pia alikuwa Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Taifa na alifariki dunia Februari 17, 2021 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alipokuwa akipatiwa matibabu, na alizikwa kijijini kwake Mtambwe, Pemba Februari 18.

Zitto aliyasema hayo jana kwenye mahojiano na kituo kimoja cha runinga jijini Dar es Salaam, na kueleza kuwa Maalim Seif alijua kwamba anapungikiwa na nguvu au Mungu kumchukua, hivyo alishaanza kuwaandaa watakaofuata baada yake.

Alisema Maalim Seif aliwaandaa watu hao kwa ajili ya kuwakabidhi majukumu ya kuendeleza aliyokuwa anayafanya hata kabla hajajiunga na chama hicho.

"Aliniita na kunieleza kwamba fulani na fulani nawaandaa kwa lolote lile linaloweza likatokea, nakwambia wewe kama kiongozi lolote linaweza kutokea… hawa ni watu ambao naamini wataweza kuendeleza hizi harakati, si mimi tu aliyeniambia hivyo, pia na baadhi ya wazee aliwaambia hivyo," alisema.

Zitto alisema pamoja na kwamba Maalim Seif aliwapa ishara ya huyo atakayeshika majukumu yake, lakini walipoangalia ishara na vigezo waliona vinatimia kabisa, na ilikuwa kazi rahisi sana kwao kufanya mapendekezo.

"Pia nawashukuru sana Watanzania wote kwa salamu zao za pole kufuatia msiba tulioupata si tu kwa chama chetu bali kwa Watanzania kwa ujumla na hasa kwa Wazanzibari," alisema na kuongeza:

"Kumekuwa na visomo vya kumwombea marehemu ambavyo vimekuwa vikifanyika sehemu mbalimbali."



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja (kulia), akiwa anashuka kwenye hoteli ya nyota 3 ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) inayojengwa wilayani Chato mkoani Geita, ikiwa ni ziara ya kikazi mkoani humo. Katikati ni Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Marufuku ujenzi wa nyumba daraja la JPM

**Na Rose Jacob,** MWANZA

SERIKALI imepiga marufuku ujenzi wa nyumba za makazi na biashara katika eneo la daraja la JPM linaounganisha wilaya za Misungwi na Sengerema, mkoani Mwanza.

Marufuku hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maendeleo na Makazi, William Lukuvi, alipozungumza na watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi. Alisema kuna watu wameanza kununua maeneo hayo kwa bei ndogo kutoka kwa wananchi upande wa Misungwi na Sengerema na kuagiza kusitishwa ujenzi wowote.

Kadhalika, Waziri Lukuvi alikagua mradi wa ujenzi wa daraja la JPM lililopo Kigongo Busisi na ujenzi wa bandari kavu ya Standard Gauge Railway (SGR) wilayani Misungwi. "Ninawaagiza watendaji wa Halmashauri ya Misungwi na Idara ya Ardhi ya Mkoa wa Mwanza kuhakikisha hakuna mtu yeyote anaendeleza ujenzi wala kununua maeneo yanayozunguka miradi ya kimkakati ikiwamo daraja la Busisi Kigongo na SGR wala kufanyika uthamini wa aina yoyote," alisema Lukuvi.

Aliitaka Halmashauri ya Misungwi kutengeneza mji wenye mpangilio katika eneo la daraja hilo na kuwalipa watu ambao wanadai fidia kwa kuwa serikali imeishaipatia Sh. milioni 300.

Aliagiza watendaji wa halmashauri zote nchini kusimamia wananchi wote wanaomiliki ardhi walipe kodi badala ya kuwatelekeza baada ya kuwapimia.

Alisema mapato mengi yakiwamo ya kodi ya ardhi yanapotea kutokana na uzembe wa watendaji hao na kuagiza kuanzishwa daftari maalum kwa kila mtaa ambalo lina majina ya wamiliki wote wa ardhi.

# Dk. Mwinyi ataka vyombo vya habari kuhubiri amani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amewataka waandishi wa habari kuzitumia vizuri kalamu zao na kwenda na malengo ya Serikali ya Zanzibar kudumisha maridhiano ya kisiasa yaliyofikiwa nchini, ambayo lengo lake ni kuondoa siasa za chuki na uhasama.

Dk. Mwinyi alisema hayo wakati alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kuzindua kongamano la habari katika kuijenga Zanzibar mpya, mjini Unguja.

Alivitaka vyombo vya habari nchini kuhubiri amani na utulivu katika kipindi hiki muhimu ambacho matunda ya maridhiano ya kisiasa yaliyofikiwa na vyama viwili vya siasa yameonekana na kufungua milango ya ushirikiano kwa serikali na sekta binafsi.

Alisema maridhiano yaliyofikiwa sasa yanatoa nafasi kubwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza malengo yake ya kufikia uchumi wa bluu na uwekezaji wa sekta mbalimbali za kitaifa.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunawaomba waandishi wa habari kuzitumia vizuri kalamu zenu kwa ajili ya kuelimisha na kuhamasisha maridhiano ya kisiasa yaliyofikiwa...matunda ya maridhiano tumeyaona ambayo ni kurudi kwa amani na utulivu wa wananchi wetu kuwa kitu kimoja," alisema.

Aliitaja mikakati mingine inayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya nane ni uwajibikaji na kupambana na rushwa na uhujumu wa uchumi.

Alisema katika kipindi kifupi cha siku 100 amefanya kazi kubwa katika kujenga uwajibikaji serikalini hatua ambayo kwa kiasi kikubwa imerudisha nidhamu ya watumishi serikalini.

"Ndugu waandishi wa habari katika kipindi cha siku 100 tumefanya mambo mengi ikiwamo uwajibikaji wa watendaji wetu pamoja na vita dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi...haya yote nawaomba waandishi wa habari wayafanyiye kazi vizuri," alisema.

Aliwataka waandishi wa habari kubadilika na kufanya uchambuzi wa matukio mbalimbali kitaalamu zaidi ambazo zinaonekana kufanywa na mitandao ya kijamii.

Alisema wananchi wanapaswa kufahamu kazi zinazofanywa na serikali na malengo ya kukuza uchumi na maendeleo kuliko kutoa taarifa za matukio ya kila siku yanayofanyika.

Alisema katika kipindi cha siku 100 tangu alipoingia madarakani amebaini hakuna mfumo mzuri wa kuzipokea taarifa mbalimbali za wananchi kutoka chini.

"Ndiyo maana nimeanzisha mfumo wa kuwasiliana na rais "sema na rais" kwa lengo la kuwawezesha wananchi kupata taarifa zao moja kwa moja na kuratibiwa na ofisi yangu," alisema.

Alisema uandishi wa habari ni kazi ya taaluma ambayo haiwezi kufanywa na kila

Naye Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Mwita Maulid, aliwataka wasemaji wakuu wa wizara kutoa taarifa kwa waandishi wa habari ili wananchi waweze kujua kazi nzuri zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya nane.

# Mfumo kudhibiti ajali barabarani rasmi

**Na Mary Geofrey**


KATIKA kuunga mkono juhudi za serikali za kupambana na ajali za barabarani, kampuni ya usafiri kwa njia ya mtandao nchini Bolt, imezindua mfumo mpya unaoruhusu madereva kufanya kazi kwa muda usiyozidi saa 12.

Mfumo huu unalenga kupunguza ajali za barabarani zinazotokana na uchovu wa madereva na kuhakikisha kuwa madereva wote wanafika kazini wakiwa wamechangamka.

Meneja wa Bolt nchini, Remmy Eseka, akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu huduma hiyo, alisema mfumo huo wa saa 12 pia utawapatia madereva muda wa kutosha wa kufanya mambo mengine muhimu kama kujumuika na familia na kujiendeleza kibiashara na kielimu. "Mfumo huu wa usalama barabarani ni sehemu ya juhudi zetu kuboresha huduma kwa faida za madereva na wasafiri ambao ni muhimu kwa biashara yetu. Kuboresha mazingira ya kimwili na kiakili kwa madereva na wasafiri ni muhimu ili kuhakikisha wote wanafika salama popote wanapokwenda.

"Ni imani yetu pia kuwa mfumo huu mpya utapunguza matukio ya ajali za barabarani na kuboresha uhusiano kati ya madereva na wasafiri," alisema Esaka.

Alifafanua kuwa mfumo huo unaruhusu dereva kufanya kazi kwa saa 12 pekee, na baada ya muda huo kupita, atazuiliwa kutumia mtandao huo na atalazimika kupumzika kwa muda uliowekwa kabla ya kuruhusiwa kurejea kutoa huduma.




## 'Ukomo mifuko plastiki iliyosajiliwa Aprili'

**Na Christina Mwakangale**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewatahadharisha wafanyabiashara, watumiaji wa mifuko ya plastiki isiyosajiliwa, kuzingatia ukomo wa matumizi hayo, mapema mwezi ujao.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Alibainisha kwamba kwa ambao watakiuka katazo la matumizi ya mifuko hiyo, adhabu ni pamoja na faini ya Sh. 30,000 hadi 200,000 kutegemeana na kosa.

Pia alisema kuwa wazalishaji wakubwa wa bidhaa za vifungashio vya plastiki ikiwamo viwanda adhabu ni kuanzia faini ya shilingi milioni tano kutegemeana na aina au ukubwa wa kosa.

"Desemba 31, mwaka jana, NEMC, tulikumbusha kuhusu kanuni kwamba vifungashio ambavyo havijakidhi vigezo visionekane katika mazingira. Ili kwa wanaotumia vifungashio na kutengeneza kwa wingi wasajiliwe au kupewa maelekezo," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema lengo la kanuni na katazo hilo ni kulinda mazingira na kuwa endelevu kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Dk. Mafwenga alisema kanuni iliwekwa ili kulinda mazingira, kupunguza uchafuzi kutokana na mifuko ya plastiki ambayo haiwezi kurejelezwa ambayo haiozi isiyooza ardhini kwa takribani miaka 400 hadi 500.

Alisema wanaozalisha vifungashio wana wajibu wa kuzirejesha bidhaa zao viwandani ili kulinda mazingira na kwamba wajasiriamali na wafanyabiashara wageukie matumizi ya mifuko ya karatasi na katani kwa kuwa kuna viwanda vinavyozalisha nchini.

## Vituo vya afya Lindi vyakabidhiwa vifaa

**Na Mwandishi Wetu, LINDI**

VITUO vya afya vya Pangaboi na Mtama vya mkoani Lindi vimepatiwa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 10.

Lengo la msaada huo uliotolewa na Benki ya NMB ni kusaidia kuboresha huduma za afya. Vifaa hivyo ni vitanda vya kujifungulia 4, vitanda vya wagonjwa 2, viti vya magurudumu kwa ajili ya wagonjwa 2, mashuka 20 na magodoro.

Vifaa tiba hivyo vilikabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, huku Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye akishuhudia na kusema kuwa msaada huo ni kielelezo kuwa NMB ni rafiki wa karibu katika kusaidia afya na elimu wilayani humo.

"Nimekuwa nikitembea maeneo mengi wilayani hapa kupokea misaada mbalimbali ya NMB katika sekta ya afya na elimu, na katika hili naomba niwashukuru sana," alisema Shaibu. Nnauye, alishukuru Benki ya NMB kwa kuwa ya kwanza kupeleka tawi katika halmashauri hiyo na pia kutoa msaada kwa kituo hicho cha afya.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Mtama, Wahida Omary, alisema anashukuru NMB kwa kuwasaidia vitanda vya kujifungulia vitakavyosaidia wazazi. Alisema zahanati hiyo inazalisha wanawake 300 kwa mwaka na kuwapo kwa kitanda kingine ni msaada mkubwa kwao.

Meneja wa NMB Lindi, Shaaban Kassari, alisema wametoa vifaa tiba ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za wadau wake wakubwa kukabili changamoto za jamii ili kuwapo na ukuaji mzuri wa kiuchumi kwa kusaidia sekta za afya na elimu.

Alisema changamoto za sekta ya afya kwa NMB ni jambo la kipaumbele, kwa kuwa afya ndio msingi wa uchumi na uzalishaji mali ni kichocheo kikuu cha maendeleo ya wananchi.

# Wanafunzi 1,800 wapewa taulo za kike

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

WANAFUNZI 1,800 wa shule za sekondari 16 za kutwa zilizopo Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, wamepokea taulo za kike zitakazosaidia tatizo la kukosa masomo wanapokuwa kwenye hedhi.

Wakizungumza baada ya kupokea taulo hizo kutoka shirika lisilo la kiserikali linaloshughulika na masuala ya afya ya lishe mkoani Kagera, walisema hapo awali kulikuwa na tatizo la kushindwa kujiamini na kuamua kukaa nyumbani hadi siku za mzunguko wa hedhi ukamilike.

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Kagemu, Devotha Faustine, alisema wanafunzi wa kike wanapokuwa katika hedhi wanasumbuliwa na tumbo na mgongo wakati mwingine hushindwa kufika darasani kabisa. "Unakuta unakosa amani nikiwa hivyo kwani natumia vitambaa ambavyo ukikaa muda mrefu unapata miwasho na kuchafua sketi, sina uwezo wa kununua pedi," alisema Faustine. Mwanafunzi wa kidato cha tatu Shule ya Sekondari Rwamishenye, Jackline Gerald, alisema akiwa kwenye hali ya hedhi mahudhurio darasani ni madogo na kupoteza masomo kwa kukaa nyumbani.

"Sio kwamba napenda niwe hivyo, lakini inanilazimu kukaa nyumbani shuleni naogopa kuaibika kwani nasoma shule ya kutwa tena yenye mchanganyiko wavulana na wasichana," alisema Gerald.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kagemu, Loyce Ngeleja, alisema kwa pindi cha mwezi mzima mahudhurio ya wanafunzi wa kike yapo chini.

"Unakuta mtoto wa kike anakosa darasani kwa muda wa siku saba zote ukifuatilia kwa undani ni hali hiyo na kweli mzazi hana uwezo wa pedi anatumia vitambaa akiwa shuleni hajiamini kabisa," alisema Ngeleja. Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali lenye kushughulikia masuala la afya ya lishe, Neema Lugakingira, alisema wametoa taulo 12 kwa kila mwanafunzi.

Alisema taulo hizo zitasaidia kwa kipindi cha mwaka mzima na kuongeza mahudhurio katika masomo na kumjenga mwanafunzi na kuongeza ufaulu.



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, akipiga picha kwa kutumia simu janja mfano wa pembe tatu ya utayarishaji wa lishe bora kwa lengo la kudhibiti tatizo la udumavu kwa watoto juzi, alipotembelea Chuo cha Maendeleo ya Jamii (CDTI), Rungemba, Wilaya ya Mufindi. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# QNET yatoa angalizo kwa kampuni za madini

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI inayojishughulisha na uuzaji wa vito (QNET), imesema kuna haja kwa kampuni zinazojishughulisha na uchimbaji wa madini kuchukua tahadhari kuhakikisha kuwa mzunguko wa thamani unafanyika kwa ubora mkubwa na uendelevu wa sekta ya vito.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo, Malou Caluza, alisema sekta hiyo imekuwa ikisaidia idadi kubwa ya watu duniani kuwapatia ajira na kukuza uchumi kwenye nchi mbalimbali, hivyo kuna haja kuhakikisha inawekewa mifumo imara ili iendelee kufanyika kwa ubora zaidi.

"QNET na toleo lake jipya la bidhaa za saa, mikufu, pete na hereni zilizotengenezwa kwa vito vya tanzanite, wanashirikiana na wasambazaji ambao ni wanachama walioidhinishwa na Baraza la Uwajibikaji la Vito (RJC)), kama wadau wakubwa tunashirikiana na serikali kuhakikisha biashara hii haifanyiki kinyume cha sheria na kuboresha uwajibikaji katika mnyororo wa thamani," alisema Caluza.

Tayari wameweka malengo kuhakikisha sekta hiyo inakuwa na maadili endelevu, na kwamba wamekuwa wakishirikiana na wadau mbalimbali katika kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kukagua mnyororo wa usambazaji wa vito hivyo.

"Kampuni yetu inafanya kazi kwa ukaribu na wauzaji ambao wanafanya kazi kulingana na kanuni za RJC kuhakikisha uadilifu, utendaji, uwajibikaji na usimamizi wa mnyororo wa usambazaji unafanyika kwa mujibu wa sheria. Kufanya kazi na wauzaji wawajibikaji na wenye maadili ni jambo muhimu sana," alisema Caluza.

"Tunahamasisha kuhakikisha kila mzalishaji katika sekta hii anatoa bidhaa zenye ubora zaidi kwa sababu kuitangaza na kuongeza thamani bila kutumia nguvu kubwa."

Alisema kila mzalishaji akizingatia malengo makuu ya uzalishaji kutakuwa na matokeo chanya si tu katika taifa bali na kwa jamii pia.

# RC Mongella ataka miradi kufunguliwa

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, amewaagiza watendaji wa serikali kuwa waadilifu kwenye matumizi ya fedha za umma na kuhakikisha miradi iliyomalizika inafunguliwa na kuanza kufanya kazi.

Aidha, amewaagiza kusimamia miradi inayojengwa na serikali kwa fedha za walipakodi ili kuhakikisha inakamilika katika muda uliopangwa kwa manufaa ya wananchi.

Alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), na kwamba uadilifu katika usimamizi bado ni changamoto katika miradi hiyo, na kuamuru wakuu wa wilaya na wakurugenzi kuhakikisha kuwa miradi yote ambayo ujenzi wake umekamilika, inaanza kutoa huduma.

"Ile Hospitali ya Buchosa Mkurugenzi, mheshimiwa DC nendeni mkamalizie, imeanza kuchakaa sasa, hospitali inachakaa kabla hata haijatoa huduma popote, tuweke sawa mazingira ya hospitali na ianze kufanya kazi, na hii nilishawaambia, Misungwi pale paanze kutumika, hata Sengerema paanze kutumika pale," alisema Mongella.

# Waandishi watakiwa kujikita kwenye kanuni

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAANDISHI wa habari mkoani Mwanza wametakiwa kujifunza kanuni na misingi ili kuhakikisha wanalinda amani.

Akizungumza wakati wa kuzindua mafunzo hayo yalifadhiliwa na Taasisi ya Kimataifa ya International Women Peace Group (IWPG ) kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari mkoani Mwanza (MPC), Mkurugenzi wa Muungano wa klabu za waandishi wa habari Tanzania (UTPC), Abubakar Karsan, alisema utamaduni na amani ndiyo vitu vya msingi duniani.

Alisema waandishi watumie fursa hiyo kushiriki vvyema na kujifunza kanuni na misingi iliyowekwa ili kuleta na kuilinda amani.

Mwenyekiti wa MPC, Edwin Soko, alisema waandishi hao 15 wataendelea na mafunzo kwa njia ya mtandao kwa miezi miwili.

Aidha, Mratibu wa IWPG, Thitiwan White, alisema shirika hilo lilianzishwa nchini Korea Kusini lina matawi 100 na vikundi 200.

# Wanawake, vijana kortini kushindwa kulipa mamilioni

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

VIKUNDI 66 vya ujasiriamali vijana na wanawake vilivyokopeshwa mikopo isiyokuwa na riba katika Halmashauri ya Kahama mkoani Shinyanga vimefikishwa mahakamani kwa hushindwa kulipa kiasi cha Sh. milioni 68.3.

Fedha hizo zilikopeshwa kwa vikundi hivyo mwaka 2013/2014, lakini mpaka sasa vimeshindwa kulipa.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Kahama Mjini, Ashura Hoja, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake, wakati akitoa taarifa ya utoaji wa mikopo isiyokuwa na riba kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Alisema kuwa halmashauri hiyo imevifikisha mahakamani vikundi 66 vya ujasiriamali vijana na wanawake wanaodaiwa kiasi cha Sh. milioni 68.3 kuvishinikiza kulipa fedha hiyo kulingana na mikataba waliyoingia.

Aidha, Hoja alisema mwaka wa fedha 2013/2014 vikundi 10 vilifikishwa mahakamani, mwaka wa fedha 2014/2015 vikundi viwili vya wanawake Kazimoto na Nguvu Mpya navyo vilishtakiwa.

Alisema mwaka 2016/2017 vikundi 12 vilivyokopeshwa na kushindwa kulipa, vijana vikiwa 10 na wanawake vikundi viwili huku mwaka 2017/2018 vikundi 21 vilishindwa kulipa kiasi cha Sh. milioni 28.3, vijana vikiwa 14 na wanawake vikundi saba.




Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga (katikati), akipokea msaada wa vifaa tiba kwa ajili ya Kituo cha Afya Pangaboi pamoja na Zahanati ya Mtama Katika Halmashauri ya Mtama, wilayani Lindi, vyenye thamani ya Sh. milioni 10 vilivyotolewa na Benki ya NMB Tawi la Lindi. Kulia ni Samuel Warioba, Mkurugenzi Halmashauri ya Mtama, Nape Nnauye, Mbunge wa Mtama, Dk. Dismas Masulubu, Mganga Mkuu Mtama na Shaaban Kassali, Meneja wa NMB katika tawi hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunda yajikita uwekezaji kwenye utalii

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

WITO umetolewa kwa madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Bunda mkoani Mara, kuhamasisha wawekezaji na wananchi kuwekeza kwenye sekta ya utalii katika mji wa Bunda.

Pia wawekezaji hao wametakiwa kuweka vivutio kuvutia watalii, kwa kuwa mji huo sasa unakuwa wakitalii zaidi, ukizingatia kuwa makao makuu ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) Kanda ya Magharibi yako wilayani humo.

Wito huo ulitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, kwenye mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani, na kueleza kuwa watu mbalimbali wakiwekeza na kuweka vivutio vya utalii katika mji huo, watalii wengi watapitia wilayani Bunda, na kwenda kutalii katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa kupitia katika Geti la Ndabaka.

Aidha, alisema watalii wakipitia katika wilaya hiyo, itakuwa ni fursa kubwa kwani watanunua bidhaa mbalimbali zikiwamo za kitalii, hali ambayo itainua uchumi wa wananchi na pia itasaidia kuongeza mapato ya ndani ya halmashauri hiyo.

"Waheshimiwa madiwani hamasisheni watu wawekeze kwenye sekta ya utalii na kuweka vivutio mbalimbali kama walivyo watu wa mikoa ya kaskazini," alisema Bupilipili.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, Michael Kweka, DC huyo kwa kuleta wazo hilo zuri, na kwamba hatua hiyo itasaidia kuongeza mapato ya ndani.

Madiwani wote walilipokea wazo hilo wakisema kuwa watawahamasisha wawekezaji na wananchi kwa ujumla kuwekeza kwenye sekta ya utalii.

# Watendaji wapewa kazi ya kusimamia madawati

**Na Julieth Mkireri, MKURANGA**

WALIMU wa shule za sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani wametakiwa kuhakikisha miundombinu pamoja na madawati inatunzwa ili kuondoa kero ya uhaba inayotokea mara kwa mara.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, alipokuwa akizungumza na walimu, watendaji, waratibu na wadau wa wilaya hiyo, ambapo alikabidhi madawati 750 yaliyotengenezwa katika karakana iliyopo ofisini kwake.

Sanga alisema walimu wanatakiwa kusimamia utunzaji wa miundombinu na pia madawati ili yaweze kudumu kwa muda mrefu na kuepuka kero ya wanafunzi kukaa chini na wengine kurundikana katika darasa moja.

Aliwahakikishia viongozi hao kuwa kazi ya kutengeneza madawati ni endelevu kutokana na ubunifu wao wa kuanzisha kiwanda ofisini kwake na kutumia mbao kutoka kwenye misitu ya vijiji vyao na wafanyakazi ambao ni wahitimu wa Jeshi la Mgambo.

Sanga alitoa pongezi kwa kikundi cha wazawa "Miuranga yetu" ambao walichangia Sh. milioni 2.1 zilizotengenezea madawati 42, huku akiwasisitiza watendaji wa kata na vijiji kuendelea kushirikiana na serikali kuhamasisha wananchi kusaidia utatuzi wa kero za sekta ya elimu.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Mshamu Munde, alisema halmashauri hiyo itaendelea kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya sekta ya elimu kuanzia awali hadi sekondari

# Watakiwa kutambua vipaji vya watoto wao

**Na Rose Jacob, MWANZA**

WAZAZI na walezi wametakiwa kutambua vipaji vya watoto wao, ili waweze kuwaendeleza katika masomo na kuwafanya watimize ndoto zao.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Diwani wa Kata ya Nyamagana jijini Mwanza, Bhiku Kotecha, katika hafla ya kuwapongeza walimu kwa matokeo mazuri ya darasa la saba mwaka jana.

Kotecha alisema matokeo mazuri kwa wanafunzi hutokana na kufanya kazi kwa ushirikiano kati ya walimu, wanafunzi kujituma na nidhamu.

"Nimefurahishwa na juhudi zenu katika kazi kwani kutoa mwanafunzi bora siyo mchezo ndiyo maana nimeandaa hafla hii na nimetoa mifuko miwili ya sukari yenye ujazo wa kilo 25, jiko la gesi na ngao katika Shule ya Msingi Nyamagana kama zawadi ya kuwapongeza walimu," alisema Kotecha.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Anadoreen Rugaimukamu, alisema kuwa kati ya shule zilizopo kwenye kata 18 wilayani Nyamagana Kata ya Nyamagana imekuwa ya kwanza na kutoa mwanafunzi bora wa kwanza wa kiume wilayani humo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 2, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

Jukumu kukiinua Kiswahili sasa lisiwe 'vita' bali elimu



Ukurasa 13

Walio sokoni, mikusanyiko sasa anzeni kuvaa barakoa



Ukurasa 14

**Ripoti tabianchi ilivyoibua kitisho kikubwa kwa dunia**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# 'Nyumba za taka' zilipogeuka adui mkubwa makazi ya watu

• Vyanzo maradhi, wadudu, majitaka

UKOSEFU wa mikakati ya kukusanya na kuzoa taka kwa wakati limekuwa tatizo sugu linalokwamisha kuwa na makazi safi na mazingira salama majijini na kwenye miji mingi nchini.

Licha ya ukweli kuwa hamasa ya kufanya usafi kampeni ya kitaifa iliyozinduliwa na awamu ya tano inaendelea ikisimamiwa na wakuu wa mikoa na wilaya kwa kushirikiana na wakurugenzi wa halmashauri ili kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu kwenye usafi, kusafisha na kuyatunza mazingira ili kujiepusha na magonjwa, lakini uzoaji taka kwa wakati unatia 'nuksi' mpango huo.

Mkoani Shinyanga kampeni hiyo licha ya kufanikiwa inakwamishwa na uchelewaji wa kuzoa taka zilizokusanywa maeneo mbalimbali. Ni dhahiri kuwa si Shinyanga pekee hata katika sehemu nyingi iwe mijini na majijini mambo ni magumu.

Uchafu unakwama kwenye maghuba na kuwa kitisho kipya cha maradhi ya mlipuko hasa kwa wale wanaoishi karibu na maghuba hayo. Hivyo ni wakati wa kufanya tathmini na kuamua sehemu zinazofaa kuweka huduma hiyo badala ya kuiacha kwenye makazi ya watu.

Mathalani, ghuba la kuhifadhi taka lililopo Majengo Makaburini Manispaa ya Shinyanga limegeuka chanzo cha magonjwa baada ya kujaa taka, uchafu kuzagaa na kutawanyika kwenye makazi ya watu ambao wanalalamikia hatari ya kuibuka magonjwa ya mlipuko.

Wakazi wa maeneo hayo wana kilio kikubwa na wanalalamikia kuachwa kwenye janga la matatizo licha ya viongozi kuahidi kuwa usafi utafanyika na eneo hilo litakuwa safi na salama katika kipindi kifupi kijacho.



Ghuba la taka la Majengo Makaburini katika Manispaa ya Shinyanga, lililo kwenye makazi ya watu limeishi kwa miezi miwili bila uchafu kuondolewa. **PICHA: MARCO MADUHU**

Bakari Said ni mkazi wa Majengo Makaburini anayeishi jirani na ghuba la uchafu, anasema taka zimeishi zaidi ya miezi miwili kwenye ghuba hilo, na katika kipindi hiki cha mvua maji machafu hutiririka na kujaa kwenye maeneo yao, makazi yanajaa funza, inzi na wanyama kama panya yote hayo yakiambatana na harufu kali inayonuka muda wote.

Mwamvita Mkondo anayeishi jirani na ghuba hilo anasema wanaishi maisha ya hatari na ni janga kwa watoto wanaocheza na kutembea juu ya uchafu wa kila namna bila kujua kuwa wanaathirika.

"Tunaomba Nipashe itupazie sauti ili uchafu huu uzolewe haraka na kulinda afya zetu na watoto, kwani tupo katika hatari kubwa ya kuugua kipindupindu, kuhara damu, kuharisha, taifodi..." anasema Mkondo.

**WANAKWAMA WAPI?**

Ofisa Afya Kata ya Kambarage Manispaa ya Shinyanga, Costansia Michael, anasema uzoaji taka kwenye maghuba unasimamiwa na idara ya usafi na mazingira manispaa hiyo na kwamba jukumu la manispaa ni kutoa taarifa za uchafu unapojaa kwenye maghuba ya taka na wameshafanya hivyo.

Diwani wa Kata ya Kambarage Manispaa ya Shinyanga, Hassani Mwendapole, anasema uchafu kwenye ghuba hilo ni kero, ambapo wamesema mara kadhaa kwenye vikao vya Baraza la Madiwani, lakini halizolewi na hali inazidi kuwa mbaya.

Ameshapita mara kwa mara kwenye ghuba hilo kujionea hali halisi yeye mwenyewe, na kusikitishwa jinsi watu wa afya kutozoa uchafu huo, ambao utasababisha mlipuko wa magonjwa, na hatimaye serikali kuingia hasara ya kuanza kudhibiti tena mlipuko huo, na kuomba uchafu huo uzolewe haraka ili kunusuru afya za wananchi.

"Ghuba hili hatujui tatizo ni nini kwanini wanashindwa kuzoa uchafu, nimepita na asubuhi kuona kama limezolewa, lakini hakuna kitu, hali iko vile vile," anasema Mwendapole.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, David Nkulila, anasema ameshafanya ziara ya kutembelea maghuba yote likiwamo hilo la Majengo Makaburini, na kukuta hali ni mbaya na baada ya kuona hali hiyo aliitisha kikao na watu wa usafi na mazingira, na kutoa maelekezo uchafu huo uzolewe haraka ili kunusuru afya za wananchi, lakini anashaghaa mpaka sasa baadhi ya maeneo ni machafu.

"Nilishatoa maelekezo uchafu huo uzolewe haraka na hata kwa kukodi magari, wakati mtambo wa kuzolea taka wa manispaa ukiendelea na matengenezo, ili kunusuru afya za wananchi,"anasema Nkulila.

**CHANZO**

"Tatizo ambalo limesababisha uchafu kutozolewa kwa wakati kwenye maghuba ni kuharibika kwa mtambo wa kuzolea taka, ambao kwa sasa upo kwenye matengenezo ndiyo maana nimeagiza watumie njia nyingine ya kuzoa uchafu huo, ili zisiendelee kuzagaa kwenye makazi ya watu," anaongeza Nkulila.

Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira Manispaa ya Shinyanga, Kuchibanda Snatus, amekiri uchafu kukithiri kwenye maghuba na kueleza kuwa wanazoa kwa awamu na zamu inayofuata ni kuzoa uchafu katika ghuba la aoko kuu, Nguzo Nane na Majengo Makabulini.

Anasema ndani ya muda mfupi pengine kwenye wiki moja maghuba yote yaliyojaa uchafu yatakuwa yamesafishwa na kuwaomba wananchi waendelee kuchukua tahadhari ya kujiepusha na magonjwa ya mlipuko, wakati wakiendelea na utaratibu wa uzoaji wa taka hizo.

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Jukumu kukiinua Kiswahili sasa lisiwe 'vita' bali elimu

TAASISI zinazohusika na ukuzaji wa Kiswahili zimeanza kazi kutekeleza rai ya serikali kuwa lugha hiyo ipewe nafasi kubwa zaidi katika utendaji na uendeshaji wa masuala ya serikali kwenye sekta ya umma.

Moja ya maeneo yaliyotajwa ni kutafsiri sheria zilizopo kwa Kiswahili na kwa maana hiyo kuwasilisha miswada ya kisheria bungeni kwa Kiswahili, badala ya kutafsiri miswada hiyo.

Bado ni mapema kusema mabadiliko hayo yatachukua kasi gani, na katika miaka miwili au mitatu ijayo kutakuwa na mabadiliko na mafanikio kiasi gani.

Kimsingi hitaji la kukuza Kiswahili si geni kwa taifa au uendeshaji wa shughuli za serikali kwa jumla, ambao umepiga hatua katika maeneo mengi. Ila ni katika awamu hii nafasi ya Kiswahili imekuwa ikiongezeka kwa kasi na hakuna uhakika kuwa kuna uhusiano halisi kati ya ukuzaji huo wa matumizi ya hitaji la uwasilishaji wa mada husika, kwa maana ya jitihada ya kueleweka. Kinachoonekana ni kuwa tunapenda tuwe tunasikika kwa Kiswahili na si tuwe tunasikika tu.

Kubadilisha lugha ya kidiplomasia kuwa Kiswahili ni jambo ambalo halina tatizo kwani tayari Umoja wa Afrika (AU) ulishakubali kuanzia 2014 kuwa Kiswahili ni moja ya lugha za kutumiwa katika shughuli rasmi za AU.

Hivyo wakuu wa nchi au wawakilishi wao wanakuwa na uhuru wa kuchagua watumie lugha ipi, na inavyoelekea kutakuwa na msisitizo wa Kiswahili kwa kipindi cha miaka kadhaa inayokuja, katika aina fulani ya majaribio.

Ni aina ya majaribio kama zilivyo sera nyingine, hivyo endapo italeta matatizo au kupunguza tija itabidi kurekebishwa na mara nyingine inachukua muda kukiri hivyo.

Tafsiri za uhitaji halisi wa mabadiliko hayo zinatofautiana na uwakilishi wake au uwasilishaji wa mada hiyo mbele ya hadhara tofauti za kiutawala unategemea anayezungumza na hisia zake katika suala hilo. Aina tatu za msisitizo au mwelekeo wa tafsiri hizo zinaonekana, moja ni ya Rais John Magufuli, ya pili ni ya makamu wake, Samia Suluhu Hassan na nyingine ni ya Jaji Mkuu Ibrahim Juma. Zote zinalenga kuinua Kiswahili ila kwa misisitizo tofauti, na hivyo tafsiri maridhawa ni kwa kiasi gani raslimali za nchi na maelekezo kiutawala zinahitaji kuelekezwa katika suala hilo ili zoezi lipimwe kwa vigezo gani.



Waziri wa Katiba na Sheria, Mwigulu Nchemba, wizara yake ina jukumu la kutafsiri sheria zote kwa Kiswahili na kuzitumia kutoa hukumu mahakamani.**PICHA: MTANDAO**

> Tanzania ni sehemu ya nchi za Jumuiya ya Madola ambako tafsiri za kisheria, hukumu zinaoana au kufanana.

Msisitizo wa JPM katika suala hilo unaelekea katika uzalendo, kuwa Watanzania wanahitaji kuienzi lugha yao, kwa kuchukua hatua kuipa kipaumbele katika shughuli za umma ndani na hata katika uwakilishi nchi za nje kwani Kiswahili kinakua katika maeneo mengi.

Katika maelezo yake, Makamu wa Rais Samia aligusia zaidi haki ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili kusikilizwa katika lugha hiyo kwenye mashauri yoyote yale, kwa maana kuwa pale ambapo hakikutumika, haiwezekani asiyejua lugha hiyo akapata haki yake au akafuatilia ni vipi kesi yake inatazamwa na kusikilizwa akirejea mienendo ya mahakamani.

Licha ya kuwa hoja hiyo ina mashiko kimsingi, ukimsikiliza Jaji Mkuu unapata picha tofauti, kuwa suala la wahitaji wasiojua lugha nyingine ya kitaaluma ila Kiswahili kusikilizwa kimsingi ni dogo, kwani usikilizaji wa mashauri yanayogusa wananchi wa kawaida katika Mahakama ya Mwanzo unaendeshwa kwa Kiswahili.

Yako maeneo mengi pia ambapo Kiswahili kinatumika katika mahakama za juu zaidi kwa mfano za wilaya au hakimu mkazi katika kesi za jinai.

Inapokuja katika masuala ya biashara na ndiyo mengi zaidi katika kesi za madai, walengwa au wahusika ni wa matabaka ya juu zaidi.

Kwa maana hiyo hata katika mahakama za ngazi ya kati Kiswahili kina nafasi yake, ila hukumu zinakuwa katika lugha ya kitaaluma kurahisisha rejea kwa mahakimu au majaji, katika muktadha unaooanisha moja kwa moja hukumu husika na dhamira ya kisheria, nini kiliamuliwa.

Kuondoa 'uteja' huo kwa Kiingereza na kuhamia Kiswahili ni kama kusema kuwa rejea hiyo haihitajiki, mahakimu hapa nchini na hivyo hata majaji wasihitaji hukumu au hisia kuhusu vipengele vya sheria husika kutafsiriwa kwingine.

Tanzania ni sehemu ya nchi za Jumuiya ya Madola ambako tafsiri za kisheria, hukumu zinaoana au kufanana.

Kwa mkereketwa wa kutumia Kiswahili kama hazina ya taifa, suala la kutunza rejea na tafsiri sahihi ya kipengele cha sheria ni dogo tu.

Ni kutojali kama mfuatano wa tafsiri ya sheria tuseme ile ya ushahidi, kipengele cha ushahidi hakimu alioutilia shaka, licha ya kuwa alifikia uamuzi kuwa hauvurugi kosa la mshtakiwa, kinafaa kumsaidia mshtakiwa (benefit of doubt).

Endapo hukumu zitaandikwa moja kwa moja kwa Kiswahili si ajabu rejea hizo zianze kupotea, hivyo ibakie tu kusema 'hakuna shaka' au 'upande wa mashtaka ulisema hakuna shaka.' Hapo viwango halisi vya utetezi na utoaji haki hushuka.

Kimsingi huo ndiyo 'muktadha' wa mjadala wa kutumia Kiswahili katika shughuli muhimu za nchi, na suala la kuweka hadharani tafsiri hazitabadili chochote katika tatizo hilo. Jambo la msingi hapo ni kuwa tafsiri hizi hazitokani na kuundwa kwa maneno ya Kiswahili na watumiaji wenyewe, kwa mfano hitaji la 'ku-scan app ya QPR' ya mtandao fulani, unaopeleka fedha kwa simu za mkononi likihusishwa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) litatunga mlolongo wa maneno kuondoa 'ku-scan' na pia 'app' isiwepo, na 'QPR' ambayo pia si Kiswahili.

Ni hali ya kutazamia watu kuanza kukariri mlolongo wa maneno mengi yatakayotungwa na BAKITA, itakayokwama.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Walio sokoni, mikusanyiko sasa anzeni kuvaa barakoa

WAFANYABIASHARA kwenye masoko ya Dar es Salaam, wanasema licha ya kuwapo corona na wananchi kushauriwa kuchukua tahadhari kinachowakwamisha kuvaa barakoa ni joto na kukosekana hewa ya kutosha kwenye maeneo yao.

Wanayasema hayo wakizungumza na Nipashe hivi karibuni. Wafanyabiashara wa Kariakoo Shimoni, ambao wote hawavai barakoa, wamerundikana sehemu moja na kukaribiana, wakizungumza muda wote, kucheka, kupiga chafya na kukohoa huku wengine wakila na kunywa, wanasema kuna joto kupindukia wakati wote na wakizivaa wanakosa hewa.

"Tunakosa pumzi, kuumwa kichwa, kuhisi vichomi na hata kujisikia kichefuchefu. Tunafanye nini hakuna feni wala madirisha makubwa ya kuingiza na kutoa hewa ya kutosha. Tunamtegemea Mungu," anasema Simon Temihanga, anayeuza matunda yanayotoka Iringa na Mbeya.

Wanasema wanapenda kujilinda wenyewe na jamii ya wafanyabiashara, lakini hawana cha kufanya mbali na kunawa mikono na kutumia vitakasa mikono.

"Tulitarajia kupata maelekezo kutoka kwa maofisa afya pengine tufanyeje kuhusu kushindwa kuvaa barakoa au serikali itoe mwongozo wa kutengeneza barakoa tofauti ambazo zinaweza kusaidia kupumua kwenye maeneo ya joto kama yetu, lakini hatujawasikia, tulitegemea labda kutakuwa na mapangaboi mengi kuongeza hewa hatujayaona..." anaongeza Temihanga.

Wanapoulizwa suala la kukaribiana bila kuzingatia umbali wa zaidi ya mita mmoja kati ya mtu na mtu wanasema tangu mwanzo walikuwa wakifanyabiashara bila kujali umbali na meza zao zimepangwa karibu karibu hivyo ni vigumu kubadilisha utaratibu uliopo bila maelekezo ya wasimamizi, au wenye soko, anasema Paulina Ndumbiko, anayeuza mboga.



Barakoa za vitambaa zimeshika kasi maeneo mengi, lakini wafanyabiashara hasa wa sehemu zenye mikusanyiko mikubwa Dar hawajahamasika kuzivaa. **PICHA: MTANDAO**

### MAELEZO YANAYOCHANGANYA

Wafanyabiashara wa mitumba wanapoulizwa sababu ya kukwepa barakoa na kuendelea kukaribiana huku wakipiga kelele za kuita wateja wanasema:

"Kuwapo maelezo mengi kuhusu corona, kunatufanya tushindwe kuamua kipi sahihi cha kufanya. Tulisikia Desemba, mwaka jana, watu 3,000 walifariki dunia kwa siku huko Marekani. Tunafahamu ni taifa lililoendelea kuna barakoa tena zenye viwango. Italia nako walifariki watu zaidi ya 1,000 kwa siku, kukaa mbalimbali na kutakasa mikono hakukufanyika. Tunajiuliza ilikuwaje?" Anahoji Simon Chuga anayeuza mitumba kwenye kituo cha mabasi cha Msimbazi.

Ananukuu taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO) kuwa watu wanaotakiwa kuvaa barakoa ni wagonjwa na wanaoonyesha dalili za corona na wahudumu wakiwamo madaktari, wauguzi na watu wengine wanaowahudumia watu wanaodhaniwa kuwa na virusi vya corona kwa hiyo wanazidi kujiuliza maswali mengi wanaposikia kuhusu vifaa kinga hivyo.

Anasema pamoja na kufahamu taarifa za corona wameelezwa kuwa kinachoumiza wengi ni kushindwa kupumua, hivyo kama mtu atashindwa kupumua atahitaji kutumia mashine na kulazwa hospitalini, lakini iwapo hujafikia hatua hiyo, unaweza kutumia dawa na kujitibia nyumbani na maisha yakaendelea.

"Sisi tunajua wanaoshindwa kupumua ndiyo wana tatizo kubwa, lakini tunaamini wengi hatutafikia huko ndiyo maana maisha yanaendelea," anasema Chuga.

Akiwa kwenye soko la mitumba Karume lililoko Ilala, Dominic Kisoki, anaiambia Nipashe:

"Hatuwezi kuvaa barakoa kazi yetu inayotupa chakula ni mdomo. Ni lazima kupiga kelele muda wote kukaribisha wateja. Kutaja bei, kutangaza sifa mbalimbali ya bidhaa kuanzia fasheni, siku zilipofunguliwa na kuita wateja. Hufanyi hayo ukiwa umeziba mdomo na barakoa."

Kadhalika wanasema kwa sababu wanategemea maelekezo na hamasa kutoka kwa viongozi kuzungumzia suala hilo ni vyema maofisa afya, wataalamu wa magonjwa ya milipuko kutoka hospitalini na hata wanasiasa kuwatembelea na kuwaelezea kuhusu maradhi hayo.

Anashauri viongozi waonekane wakitembelea masokoni kwenye misongamano hasa Kariakoo, wakuu pamoja na redio hasa ya sokoni hapo ikitumiwa kuwahamasisha wafanyabiashara ndogondogo kujihami na ugonjwa huo.

Watu wana maswali mengi viongozi hasa wataalamu wa afya wanaweza kukutana na wafanyabiashara wachache wachache na kujibu maswali yao na kuwatolea hofu na kuwapa ufafanuzi kuhusu umuhimu wa barakoa na kuweka mipango ya kujipanga na kukaa mbalimbali ili kupunguza kasi ya kusambaa magonjwa.

Wanaomba serikali kutengeneza barakoa zinazoweza kutumiwa maeneo yenye joto zaidi na mikusanyiko mikubwa.

> Majimaji za mwili zenye virusi huingia kwa njia ya hewa kutoka kwa waathirika kupitia kuongea, chafya na kukohoa iwapo una barakoa inayoziba pua na mdomo unaweza kubaki salama.

### UMUHIMU WA BARAKOA

Licha ya maelezo mengi kutolewa kuhusu corona, watafiti wanasema ugonjwa huambukizwa kwa njia za hewa kama kupitia puani na mdomoni wakati wa kuongea, kupiga chafya na kukohoa.

Shirika la Utangazaji la BBC linaeleza kuwa virusi vya corona vinaweza kusambazwa kwa matone ambayo yanakaa hewani, pale ambapo wale walioambukizwa wakiongea, wakikohoa au kupiga chafya. Virusi hizo vinaweza kuingia mwilini kupitia macho na mdomo au puani au kugusa vitu vilivyopata maambukizi ndiyo maana wataalamu wanashauri kuwa iwapo watu watavaa barakoa haya matone ya virusi yanaweza kupunguzwa.

Majimaji za mwili zenye virusi huingia kwa njia ya hewa kutoka kwa waathirika kupitia kuongea, chafya na kukohoa iwapo una barakoa inayoziba pua na mdomo unaweza kubaki salama.

BBC inasema virusi vikishatoka kwenye majimaji za walioathirika hushuka chini na kama watu watakaa umbali zaidi ya mita moja wanapozungumza uwezekano wa kuwafikia na kuingia kupitia mdomoni au puani ni mdogo.

Aidha, wanakumbushwa kunawa mikono mara kwa mara au kutumia vitakasa mikono hasa sehemu ambazo hazina maji na kuacha mazoea ya kushika pua, macho na midomo kwa vile unaweza kujiingizia virusi midomoni.

SAYANSI

**NA MWANDISHI WETU**



Uchafuzi wa mazingira unaotokana na uzalishaji usiojali mazingira unakwamisha jitihada za kupunguza kiasi cha joto duniani. **PICHA: UN NEWS**

# Ripoti tabianchi ilivyoibua kitisho kikubwa kwa dunia

KATIKA hali inayoashiria kuwa mambo siyo mazuri kwenye kukabiliana na joto duniani, Umoja wa Mataifa (UN) umeeleza kuwa mataifa hayajafikia popote kupunguza kiwango kinachotakiwa kukabili ongezeko la joto duniani.

Ripoti mpya ya Umoja wa Mataifa iliyotolewa jana ilizisihi serikali kuchukua hatua madhubuti na za kina ili kufikia malengo ya mkataba wa Paris wa mabadiliko ya tabianchi kuhakikisha ongezeko la joto duniani linadhibitiwa na halizidi nyuzi joto 1.5 katika kipimo cha 'selsiyasi' au 'sentigrade' ifikapo mwishoni mwa karne hii.

Ripoti hiyo ya awali ya uchambuzi ilitolewa na sekretarieti ya mkataba wa kimataifa wa mabadiliko ya tabianchi (UNFCCC) kuhusu viwango vya nchi kuchangia kukabili mabadiliko ya tabianchi, (NDCs), imekuja kabla ya mkutano wa 26 wa nchi wanachama wa mkataba wa mabadiliko ya tabianchi (COP26) utakaofanyika Novemba, mwaka huu, huko Glasgow Ireland.

Aidha, ripoti imebainisha kuwa hata baadhi ya nchi zikiongeza juhudi, bado kwa ujumla kile kinachotakiwa hakitafikiwa.

"Leo ripoti ya mpito ya UNFCCC inatoa onyo kwa sayari yetu. Inaonyesha kuwa serikali bado hazijafikia popote kukaribia kiwango kinachotakiwa cha kuhakikisha ongezeko la joto halizidi nyuzijoto 1.5 katika kipimo cha selsiyasi kwa mujibu wa mkataba wa Paris," anaonya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, António Guterres, akichangia ripoti hiyo.

> "Sayansi iko bayana, kudhibiti kiwango cha ongezeko la joto kisizidi nyuzijoto 1.5 lazima tupunguza hewa chafuzi kwa asilimia 45 ifikapo mwaka 2030 kutoka viwango vya mwaka 2010.

### 2021 KUJENGA AU KUBOMOA

Katibu Mkuu Guterres anasema mwaka huu wa 2021 ni wa kujenga au kubomoa katika kukabiliana na dharura ya mabadiliko ya tabianchi.

"Sayansi iko bayana, kudhibiti kiwango cha ongezeko la joto kisizidi nyuzijoto 1.5 lazima tupunguza hewa chafuzi kwa asilimia 45 ifikapo mwaka 2030 kutoka viwango vya mwaka 2010." Anasisitiza Guterres.

Katibu Mkuu anatoa wito kwa wachafuzi wakuu kuongeza viwango vyao vya kupunguza utoaji wa hewa hizo chafuzi kwa kumulika malengo ya mwaka 2030 kwenye NDCs zao akiangazia janga la COVID-19 anasema mipango ya kujikwamua kutoka katika janga hilo in fursa ya kujenga dunia inayolinda na kuhifadhi mazingira.

"Watoa maamuzi lazima watekeleze ahadi zao. Waliyoahidi kwa muda mrefu ni lazima yaendane na vitendo vya kuzindua muongo wa mabadiliko ambao watu na sayari wanahaha kupata," alisema Katibu Mkuu.

### ILICHOMULIKA RIPOTI

Ripoti hiyo ya UNFCCC imejumuisha mawasilisho ya taarifa za hadi Desemba mwaka 2020, ikionyesha kuwa wanachama 75 wa mkataba huo wa UNFCCC ndiyo waliwasilisha vigezo vipya au vilivyoboreshwa vya NDCs na hivyo kuwa ni asilimia 30 tu kiwango cha hewa chafuzi inayotolewa duniani.

Katibu Mtendaji wa UNFCCC anasema kuwa ripoti hiyo ni sehemu kidogo ya hali halisi ya viwango vya nchi kukabili mabadiliko ya tabianchi wakati huu ambapo janga la COVID-19 linaleta changamoto ya wazi kwa nchi nyingi kukamilisha mawasilisho yao ya mwaka 2020.

Anasema ripoti ya pili itatolewa kabla ya COP26 itakayofanyika Glasgow na alitoa wito kwa nchi hususan zile zinazoongoza kwa hewa chafuzi na ambazo hazijawasilisha ripoti, zifanye hivyo ili taarifa zao zijumuishwe katika ripoti ya mwisho.

"Tunapongeza nchi wanachama ambazo licha ya changamoto za COVID-19 zimetekeleza wajibu wao kwa mujibu wa mkataba wa Paris na kuwasilisha viwango vyao vya kitaifa kabla ya tarehe ya mwisho, lakini naomba waliosalia watekeleze ahadi haraka iwezekanavyo," anasema Espinosa akiongeza kuwa, "Iwapo jukumu hili lilikuwa dharura awali, sasa ni muhimu kupita kiasi."

### JANGWA SAHEL KUTIBIWA

Katika jitihada za kuokoa dunia na mabadiliko ya tabia nchi, mradi kabambe wa kukabiliana na hali ya jangwa kwenye ukanda wa Sahel na Sahara unaojulikana kama Great Green Wall (GGW) ambazo ni juhudi za kimataifa za kukabiliana na jangwa na kurekebisha uharibifu kwenye mataifa yaliyo ndani ya Jangwa Sahel unaingia katika hatua nyingine baada ya kupokea ufadhili wa dola bilioni 14.236.

GGW ni mradi unalenga kurekebisha hekari milioni 1,000 zilizoharibiwa na jangwa na kubuni ajira milioni 10 zinazojali mazingira.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guteress, anasema, kwa kupanda mimea hekari milioni 1,000 zilizoharibiwa, uhakika wa chakula utahakikishwa, kaya zitabaki na ajira zitabuniwa.

Anaongeza kwamba juhuzi hizo zitarejesha bayoanuai, kupunguza makali ya mabadiliko ya tabianchi na kujengea jamii nyumbufu (mnepo) kwenye mazingira hayo ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Rais wa Mauritania Mohamed Cheikh El-Ghazouani, ambaye ni mwenyekiti wa kongamano la viongozi wa nchi na serikali la kusimamia GGW amekaribisha mpango huo kwa niaba ya ukandawa Sahel akisema, "tunakaribisha kutangazwa kwa mradi wa haraka wa Great Green Wall ambao lengo lake ni kutoa ufadhili wa kwanza katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025 ili kuhakikisha kutekelezwa kwa dhamira ya wadau wa kifedha katika utaratibu unaofaa.'

Rais Ghazouani anaongeza kwamba, "uchangishaji wa fedha zingine kupitia njia bunifu utasaidia kufikia malengo ya Great Green Wall ambao unalenga kurekebisha hekari milioni 1,000 zilizoharibiwa na mabadiliko ya tabianchi na kubuni ajira milioni 10 zinazojali mazingira."

Tangu kuanzishwa kwa mradi wa Great Green Wall mwaka 2007 umeungana na wadau wengi kwa ajili ya kuboresha mazingira ya ukanda huo na kujenga kilometa 8,000 za msitu katika nchi takriban 11 na kufikia malengo ya maendeleo endelevu ifikapo waka 2030.

Mradi huo ambao sasa uko katika muongo wa pili ni kielelezo cha kutumia nguvu asilia kwa ajili ya kutoa suluhu za kimazingira kama vile kuharibiwa kwa mazingira, kukua kwa jangwa, ukame, mabadiliko ya tabianchi, kupotea kwa bayoanuai, umaskini na ukosefu wa uhakika wa chakula.

Ukanda wa Sahel una mataifa ya Senegal, Mauritania, Mali, Burkina Faso, Algeria, Niger, Nigeria, Chad, Sudan na Eritrea. **UN NEWS**



# Mwanafunzi kortini tuhuma za rushwa

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Dodoma, imemfikisha katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma, aliyekuwa mwanafunzi wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP), Patrick Abohokile (26) kwa tuhuma za rushwa.

Inadaiwa kuwa Abohokile alishawishi kupatiwa Sh. 340,000 na kupokea Sh. 320,000 kutoka kwa wanafunzi wawili wa mwaka wa tatu wa chuo hicho waliokuwa wamefanya mtihani wa marudio wa somo la Applied Statistics II ili awasaidie kurudia kufanya mtihani huo nje ya mfumo rasmi wa chuo.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema pia imemfikisha mahakamani mwanafunzi Rufus Msemwa (32), ambaye amefunguliwa mashtaka mawili ya kuahidi na kutoa rushwa Sh. 20,000 kwa mwanafunzi mwenzake ili asaidiwe kurudia mtihani huo.

Kibwengo alisema watuhumiwa hao wamefunguliwa mashauri matatu ya kushawishi, kupokea na kuahidi kutoa rushwa kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, sura ya 329 marejeo ya 2019.

Alifafanua kuwa uchunguzi wa TAKUKURU ulibaini Novemba 2, 2020 washtakiwa wakishirikiana na watu wengine ambao bado wanatafutwa walitenda makosa hayo na kuwezesha baadhi ya wanafunzi wa mwaka watatu wa IRDP kufanya mtihani husika nje ya mfumo kinyume na taratibu za chuo.

Katika hatua nyingine, TAKUKURU imemfikisha mahakamani Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Chinugulu wilayani Chamwino, Peter Kyara (36) kwa kosa la kushawishi rushwa ya Sh. 500,000.

Alisema uchunguzi umeonyesha kwamba Desemba 10, mwaka jana, mtuhumiwa alimtaka mwananchi mmoja ampatie hongo hiyo ili asimchukulie hatua baada ya kushtakiwa kwa kosa la kuchunga mifugo kwenye shamba la mwananchi mwingine.

Aliwaasa watumishi wa umma na wengine kuwa makini na vitendo vya rushwa kwa sababu taasisi hiyo imejipanga kila mahali kuhakikisha rushwa inatokomezwa.

"Naomba jamii iwe makini na vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi ya watu, tushirikiane ili tuweze kuwafichua watu wa aina hiyo," alisema Kibwengo.

Kadhalika, alisema wanaendelea kuwaasa vijana kujiepusha na mafanikio kwa njia ya mkato badala yake wajibidiishe katika masomo na kila jambo wafanyalo liwe la halali.

Aliwaonya watendaji katika kata, mitaa na vijiji vyote mkoani hapa kujiepusha na vitendo vya rushwa na kuzingatia taratibu halali za utendaji ili wasikutane na mkono wa sheria.



Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, akishiriki kufanya usafi katika Mtaa wa Nyerere Square jijini Dodoma lililofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wafanyabiashara waaswa chuki zisizo na tija

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA Halmashauri ya Jiji la Dodoma wametakiwa kujenga uhusiano mzuri na jiji hilo ili kufanya biashara bila kubughudhiwa.

Ofisa Masoko wa halmashauri hiyo, James Yuna, alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara wa matunda, mboga, na viazi wakati akikagua masoko na kutatua kero zinazowakabili.

"Nawashauri ninyi wafanyabiashara kutumia nafasi mliyonayo kujenga uhusiano wa karibu ili mkuze mitaji yenu badala ya kutumia muda mwingi kutengeneza chuki zisizo na tija," alisema.

Yuna alisema lengo la halmashauri hiyo ni kuona wafanyabiashara wanakuza mitaji yao kwa kuzingatia sheria na taratibu.

"Halmashauri ya Jiji ipo kwa ajili yenu nyinyi wafanyabiashara na ninafurahi ninapoona mnafanya shughuli zenu kwa malengo ya kuinua mitaji yenu kutoka ngazi ya chini hadi juu, hivyo ni matumaini yetu hamtakuwa na muda wa kutengeneza uhusiano mbaya wenye kubomoa maendeleo yenu," alisema.

Aliwasihi kutii na kutekeleza maelekezo yanayotolewa na halmashauri hiyo ili kuwa na tija kwenye biashara zao. Kwa upande wao, wafanyabiashara hao wameiomba halmashauri hiyo kuwa na uhusiano wa karibu pindi wanapotoa maelekezo ya uboreshaji kwenye biashara zao, badala ya kushtukizwa.

Mfanyabiashara wa Soko la Bonaza, Goha Magwai, alisema uhusiano mwema utawajengea wafanyabiashara hao heshima kubwa ya kuepuka kufanya biashara maeneo yasiyo rasmi.

Naye Joseph Yusuph, mfanyabiashara wa Soko la Kikuyu, alisema wafanyabiashara wanatakiwa kujipanga na kufanya biashara kwa ufanisi na kutumia teknolojia ya kisasa badala ya kutumia mifumo ya kizamani ambayo imekuwa ikidumaza mitaji yao.

Yusuph alisema kutokana na maboresho yanayofanyika katika baadhi ya masoko, kuna kila sababu ya kufanya shughuli zao kwa njia ya kisasa ili kuweka ushindani.

# DC aahidi kuwatafutia ufadhili wanafunzi kidato cha IV

**Na Ibrahim Joseph, KONGWA**

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Suleiman Serera, ameahidi kuendelea kuwatafutia ufadhili wa masomo baadhi ya wanafunzi wa masomo wa kidato cha nne na sita watakaofanya vizuri kwenye mitihani yao ya kitaifa.

Dk. Serera alitoa kauli hiyo juzi, wakati alipokuwa akipokea msaada wa kompyuta tatu kutoka Benki ya NMB kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Mumi, wilayani hapa.

Alisema atawatafutia wafadhili wa ndani na nje ili kuinua kiwango cha elimu katika wilaya hiyo.

"Mwaka huu kuna baadhi ya wanafunzi wa wilaya hii nimewatafutia ufadhili wa masomo wanaendelea na masomo kwenye vyuo vya kati na wengine vyuo vikuu hapa nchini kwa ufadhili," alisema.

Alisema lengo lake la kuwatafutia ufadhili wanafunzi hao ni kuwaendeleza kielimu ili kuikomboa wilaya hiyo kielimu na kiuchumi.

Sababu ya kuwatafutia ufadhili ni baada ya kugundua kuna wanafunzi wanajitahidi kufanya vizuri kwenye mitihani, lakini wanakwama kuendelea na masomo kutokana na kukosa watu wa kuwasomesha.

"Nawaombea ufadhili wa masomo kwa baadhi ya balozi zilizopo hapa nchini ili kuwasaidia wanafunzi hao kusoma kwenye vyuo vya hapa nchini au nje ya nchi," alisema.

Aliishukuru benki hiyo kwa msaada waliotoa ambao utasaidia walimu kuandaa masomo na mitihani. "Kompyuta hizi ninyi NMB mnaona kuwa ni kitu kidogo, lakini kwetu sisi ni msaada mkubwa katika kuwasaidia walimu wetu kuandaa mitihani ya shule kwa sababu ilikuwa kikwazo," alisema.

Aliwataka wanafunzi hao kujitahidi kufanya vizuri kwenye masomo yao kwa sababu wazazi na taifa wanawategemea kusaidia katika maendeleo. Meneja wa benki hiyo Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema msaada wa kompyuta zilizotolewa ni kuwasaidia kielimu. "Tumeona tupunguze kompyuta kwenye ofisi yetu, tutajibana kutumia kompyuta chache ili kuwasaidia watoto wetu wapate elimu kwa sababu ndio viongozi wajao," alisema. Alisema wamekabidhi viti na meza 60 kwa ajili ya shule hiyo vyenye thamani ya Sh. milioni tano ili kuunga mkono juhudi za serikali kutoa elimu.



## Ulaji sahihi wa vyakula wasisitizwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFANYAKAZI wamekumbushwa kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya kwa kuhakikisha wanazingatia ulaji sahihi wa vyakula, kufanya mazoezi na kuachana na mambo yasiyofaa ili kuepukana na magonjwa.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya katika Siku ya Programu ya Ustawi wa Jamii kwa wafanyakazi wa Benki ya CRDB.

Mfune alisema wafanyakazi walio wengi hawana muda wa kufanya mazoezi hivyo kupitia programu hiyo walihamasisha kujenga utamaduni wa kupima afya zao na kufanya mazoezi ili kukabiliana na magonjwa mbalimbali.

"Mazoezi yana faida kubwa sana hasa watumishi muda mwingi wako bize kuwahudumia wananchi naomba kupitia siku hii ya afya kwa wafanyakazi wa Benki ya CRDB ili kujikinga na kupambana na magonjwa nyemelezi," alisema Mfune.

Meneja Uhusiano na Ustawi wa Wafanyakazi, Benki ya CRDB makao makuu, Crensencia Kajiru, alisema lengo ya siku ya afya kwa wafanyakazi hao ni kuwajenga kisaikolojia ili wawe sawa katika kutimiza majukumu yao.

Sambamba na hilo, pia watumishi walifundishwa namna bora ya kubadili mtindo wa maisha ambao unasababisha magonjwa yakiwamo yasiyoambukiza.

Meneja wa Benki Kanda ya Nyanda za Juu, Denis Mwoleko, alisema mbali na kufanya mazoezi ya kujenga afya, pia siku hiyo ilitumika kuwaunganisha wafanyakazi wa taasisi hiyo kutoka maeneo mbalimbali.

Alisema programu hiyo ni endelevu na itawasaidia kutimiza majukumu yao katika hali ya utulivu kwa kuzingatia taratibu na miongozo ya kazi.

Mkuu wa Kitengo cha Afya cha Benki hiyo, Timoth Fasha, alisema ni vyema watumishi hao wakajenga utamaduni wa kutembea angalau nusu saa kwenda au kutoka kazini ikiwa ni sehemu ya mazoezi.

# Mabadiliko ya tabianchi yakwaza wanawake

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIKWAZO vya kijiografia na mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na uharibifu wa mazingira, vimetajwa kuwa sababu inayokwamisha wanawake kiuchumi kutokana na kuathiri shughuli zao za uzalishaji hususani kilimo.

Hayo yalielezwa juzi na Mjumbe wa Bodi ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Jovita Mlay, wakati akizungumza na Nipashe kuelekea Siku ya Wanawake Duniani. Siku hiyo huadhimishwa duniani Machi 8.

Mlay alisema kuwa mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali hususani vijijini, yamepelekea mvua kusuasua au kukosekana kabisa na kuathiri shughuli za kilimo zinazofanywa na wanawake, hivyo kushindwa kufikia malengo yao.

Kwa mujibu wa Mlay, mvua inaponyesha kidogo au inapokosekana kabisa, inasababisha wanawake ambao wanajihisisha na kilimo kupata mazao machache na kusababisha kushindwa kuinuka kiuchumi, huku akisisitiza umuhimu wa jamii kulinda na kuhifadhi mazingira.

"Lakini katika baadhi ya kata zimekumbwa na ukosefu au upatikanaji duni wa maji... jamii zimekosa vyanzo vya uhakika vya maji na waathirika wakubwa ni wanawake, hili eneo pia liangaliwe kwa upekee," alisema.

Katika hatua nyingine, alisema pamoja na mafanikio ya kupinga ukatili wa kijinsia, lakini bado kuna mfumo dume ambao umekuwa ukirudisha nyuma juhudi za serikali katika kutekeleza mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili wa wanawake na watoto.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP-Mtandao, Lilian Liundi, alisema dhana ya usawa kijinsia ni suala la maendeleo na sio vinginevyo.

Alisema lengo ni kujenga nguvu ya pamoja na kuhakikisha rasilimali za nchi zinagawanywa katika haki na usawa ikiwa ni pamoja na familia, jamii, serikali za mitaa na Serikali Kuu zinagawanya bajeti zenye mlengo wa kijinsia.

"Kama wanawake ni zaidi ya asilimia 50, vijana ni zaidi ya asilimia 60 sidhani kama kuna mpango wowote wa maendeleo ukiwaacha nyuma utakwenda vizuri, ukiyaacha nyuma hayo makundi maendeleo yatasua sua sana hayatakwenda vizuri," alisema Liundi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Paul Ntinika, alisema serikali haitawavumilia watu wote ambao watabainika kufanya vitendo vya ukatili wa kijinsia pamoja na watoto, ukiwamo ubakaji na kuwapa ujauzito wanafunzi.




Meneja Mkuu wa kampuni ya uendeshaji joto ardhini Tanzania (TGDC), Kato Kabaka (wapili kushoto), akimkabidhi mkataba wa makubaliano ya kuanza uchongwaji wa visima vitatu vya utafiti wa joto ardhini unaotarajia kuanza katika Kijiji cha Halmashauri ya Busokelo, mkoani Mbeya, Kaimu Mkurugenzi wa STAMICO, Mhandisi Venance Mwase, jana jijini Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mbunge kutetea wakulima kuporwa mashamba

**Na Grace Mwakalinga,** MOMBA

MBUNGE wa Momba, mkoani Songwe, Condesta Sichalwe, ameahidi kuingilia kati suala la wawekezaji kuwanyanyasa wakulima wa Kata ya Kapele ambao wananyang'anywa mashamba yao kimabavu. Mbunge Sichalwe alipokea malalamiko hayo jana wakati wa kikao cha kusikiliza kero za wananchi, ambapo moja ya hoja zilizotolewa na wananchi hao, ni kunyanyaswa na wawekezaji ambao hujimegea mashamba ya mpunga kimabavu.

Alisema anakwenda kushughulikia kero hiyo kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya sheria na kwamba atakayebainika atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Aidha, aliwaomba wakulima wa Kata ya Kapele kutokubali kuachia maeneo yao ya kilimo kwa madai kuwa wana haki na waendelee na shughuli za kilimo kama kawaida, huku akiwaomba watendaji na viongozi wengine kushughulikia suala hilo. "Nimepokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa Kapele, kudai kunyanyaswa na baadhi ya watu ambao wanajiita wawekezaji, wanajimegea maeneo makubwa ya mashamba bila kufuata utaratibu, halafu wanawageuka wananchi wangu wakikutwa kwenye maeneo hayo wanapigwa na kutishiwa," Sichalwe.

Aidha, aliliomba Jeshi la Polisi kushughulikia suala hilo ikiwamo kuwakamata na kuchukua hatua kwa wawekezaji wote wanaodaiwa kuwanyanyasa kwa vipigo na kuwanyang'anya mashamba wakulima.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wialaya ya Momba, Twist Maulid, aliwaomba wananchi wa Kapele kutofumbia macho vitendo vya ukatili sambamba na kutokubali kurubuniwe kwa vipande vya fedha ili kuachia ardhi yao.



# Watendaji watakiwa kusimamia utekelezaji wa ilani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewashauri watendaji wa chama na serikali kufanya kazi kwa ushirikiano ili kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya CCM ya 2020/2025.

Hemed alitoa ushauri huo katika halfa ya kukabidhi magodoro kwa vituo vya afya vya Jimbo la Chaani, vilivyotolewa kwa ushirikiano baina ya Mbunge na Mwakilishi wa jimbo hilo, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi zao walizozitoa wakati wa kampeni.

Alisema kuna kila sababu kwa viongozi hao kushirikiana ili kusaidia serikali kutekeleza miradi mbalimbali na utekelezaji wa ilani ya CCM na ahadi zilizotolewa wakati wa kampeni.

Aliwapongeza viongozi hao wa jimbo kwa ushirikiano walioonyesha kwa kuwatumikia wananchi na kuanza kutimiza ahadi zao mapema kitendo alichosema kitasaidia kukijengea heshima chama pamoja na kutengeneza mazingira mazuri kwa chaguzi zijazo.

Akizungumzia suala la uwajibikaji kwa watendaji wa vituo vya afya na maeneo mengine, Hemed aliwataka viongozi wa chama kwa kushirikiana na kamati zao za ngazi ya mkoa na wilaya kutembelea katika vituo ili kujiridhisha na huduma zinazotolewa na watendaji.

Akijibu ombi la Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Hemed alisema serikali imetoa maelekezo kwa Wizara ya Afya kupeleka maombi maalum ya wataalamu wanaowahitaji katika sekta hiyo na serikali itatoa kibali maalum kwa ajili kufanya uajiri.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, alisema Mkoa wa Kaskazini unafanya kazi kwa ushirikiano, lakini zipo baadhi ya changamoto zinazoikabili sekta ya afya ikiwamo uhaba wa vifaa tiba, dawa pamoja na idadi ndogo ya watumishi katika kada ya afya.

Kwa upande wao viongozi wa jimbo hilo, Mbunge na Mwakilishi, walisema utoaji wa magodoro katika vituo vya afya ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025, pamoja na ahadi walizozitoa wakati wakiomba ridhaa kwa wananchi wa jimbo hilo.

Akitoa shukrani kwa niaba ya uongozi wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kaskazini, Mwenyekiti wa Mkoa huo, Iddi Ali Ame, alimhakikishia Makamu wa Pili wa Rais kuwa Chama Cha Mapinduzi kitaendeleza ushirikiano wake na serikali kwa ngazi ya mkoa na wilaya kwa ajili ya kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

Alisema Chama Cha Mapinduzi kinalaani vitendo vya udhalilishaji vilivyoshamiri katika visiwa vya Zanzibar na kuahidi kuwa chama kinaungana na serikali kupiga vita jambo hilo.



Wananchi wa Kijiji cha Bambi wakishiriki kukusanya mawe, Mkoa wa Kusini Unguja, eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa shule ili kuwaondolea adha wanafunzi ya kutembea umbali mrefu. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

# Vyama vya siasa vyatakiwa kutoa fursa kwa mwanamke

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

VYAMA vya siasa vimeshauriwa kuweka mifumo rafiki katika vyama vyao itakayotoa fursa kwa mwanamke kugombea nafasi mbalimbali za uongozi bila vizuizi kama ilivyo hivi sasa.

Viongozi wa vyama vya siasa walio katika ngazi ya matawi, wadi pamoja na majimbo, walitoa rai hiyo walipokutana katika majadiliano ya kuwawezesha wanawake katika uongozi yaliandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), upande wa Zanzibar yaliyofanyika Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Walisema bado mifumo na Katiba ya baadhi ya vyama havijawa rafiki kwa mwanamke kugombea nafasi za juu za uongozi hali inayosababisha muda mwingine kudhani kugombea nafasi ya uongozi ndani ya chama ni kujidhalilisha.

Mmoja wa wachangiaji, Thuwaiba Mohamed, ambaye aligombea nafasi ya uwakilishi katika uchaguzi uliopita wa mwaka 2020 kupitia Chama cha ACT -Wazalendo, alisema hata katika fomu kuna baadhi ya vipengele vya kujieleza vinavyoweza kumvunja moyo mwanamke. "Kuna baadhi ya vipengele utaona vinauliza kwa nini wewe mwanamke umeamua kugombea nafasi hii, kama mwanamke unajiuliza ina maana wanawake sisi hatuwezi kwanini hawakuweka kwa wanaume, hivyo mwenyewe binafsi kama huna ujasiri unaweza kujikatisha tamaa," alisema.

Alisema changamoto nyingine ni wanaume waliopo katika vyama hawaamini kama mwanamke anaweza akashika uongozi wa ngazi ya ubunge au uwakilishi na hata muda wa kupitisha mgombea ndani ya chama wanawake wanavunjwa moyo.

"Utaona ndani ya chama wanaume ndio wanakuvunja moyo, wanasema haiwezekani kwa hali ya uchaguzi tumuweke mwanamke, atazungumza nini mbele ya jamii na siasa za kwetu zinajulikana hii pia ni changamoto za wanawake," alisema.

Naye Haji Mohamed Ali kutoka Chama cha ACT-Wazalendo alisema bado mifumo ya vyama vya siasa haijaweza kumsaidia mwanamke kwa asilimia kubwa kama taswira ya dunia inavyohitaji juu ya usawa kwa wanawake.

Alisema kutokana na hali hiyo imesababisha wanawake kukimbilia viti maalum, huku baadhi yao wakiwa na wanauwezo mkubwa wa kuzungumza na kuishawishi jamii ikilinganishwa pengine na hata hao wanaume.

Kwa upande wake Mwakilishi wa CHADEMA, Omar Khatib, alisema hivi sasa ndio muda muafaka wa vyama vya siasa kufanya marekebisho ya mifumo ya vyama ili penye uzito pawekwe wepesi kumpa fursa mwanamke kugombea katika uchaguzi wa mwaka 2025.

Majumbe wa Sheha wa Shehia ya Nungwi Nachum Massoud, alisema katika jamii ya Zanzibar bado kuna maeneo kumsimamisha mwanamke kugombea nafasi ya uongozi inakuwa ngumu ikilinganishwa na maeneo mengine.

Mwezeshaji katika mdahalo huo Yumna kutoka Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAZA), alisema licha ya chagamoto wanazopitia wanawake, bado wanafursa ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika maeneo yao kuanzia ngazi za shehia hadi za kitaifa. Alisema katika uchaguzi wa mwaka 2020 wanawake wengi walijitokeza kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya urais kwa Zanzibar hususani katika Chama Cha Mapinduzi, lakini kati ya hao hakuna hata mwanamke mmoja aliyeingia hatua ya tano bora.

## Kampuni yatoa magari 5 ya kuzoa taka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohamed, amesema kupatikana kwa magari matano ya kuzoa taka kutayawezesha mabaraza ya manispaa kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa na kuiweka miji ya Zanzibar katika hali ya usafi.

Aliyasema hayo mjini Zanzibar wakati akizungumza baada ya makabidhiano ya magari matano ya kubeba taka yaliyotolewa na Kampuni ya Rom Solution yenye thamani ya Euro 160,000 na kati ya hayo matatu yatapelekwa kwa Mabaraza ya Manispaa ya Unguja na moja Pemba.

Mohamed alisema litakuwa ni jambo la kushangaza kuona vitendea kazi kwa ajili ya usafi vimepatikana, lakini watendaji au wasimamizi wa mabaraza ya manispaa wakashindwa kutekeleza wajibu wao vilivyo katika suala la usafi.

"Msaada huu wa magari haya utakuwa hauna maana tukishindwa kuyafanyia kazi iliyotarajiwa, niwaombe sana wasimamizi kutekeleza wajibu wenu ipasavyo ili wahisani wetu nao waone jitihada zetu," alisema.

Alisema serikali haitakuwa tayari kuona watendaji wa aina hiyo, ambao ni tegemeo la kuifanya Zanzibar kubadilika katika suala la usafi, lakini wakashindwa kusimamia vyema kazi hiyo.

"Kwa kuwa suala la usafi ni jambo la muhimu kuna haja ya kufanyika kwa tathmini kila muda ili kuona kama kuna changamoto iweze kutatuliwa, ili lengo letu la kuifanya Zanzibar kuwa ya kuvutia katika suala la usafi liweze kutimia," alisema.


Waziri Mohamed aliwataka watendaji waliopewa dhamana kusimamia majukumu yake ili kuleta matokeo mazuri kwa maslahi ya taifa.

Naye Mkurugenzi wa kampuni hiyo ya Rom Solution kutoka nchini Romania, George Alexandru, alisema msaada huo ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Serikali ya Zanzibar katika suala la usafi.

Alisema kampuni yao itaendelea kutoa msaada kama hiyo kila hali inaporuhusu, katika sekta mbalimbali lengo likiwa kudumisha umoja na ushirikiano uliopo katika pande mbili hizo.

# MATANGAZO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MUKURASI DOMITIAN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.3861-0041 kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **ANDERLEK RIDGE SEKONDARI** mwaka 2009. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/OST/RB/109060/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 31 LA 2021**
**Maombi ya barua ya usimamizi wa mirathi ya marehemu**
**BRETHA DAUDI MSALILWA MAREHEMU**
**DHIDI YA**
**GENY DAUDI MSALILWA MWOMBAJI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya **tarehe 25 mwezi 3 mwaka 2021**

**Hati hii imetolewa 25 mwezi 2 mwaka 2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO – MKUYUNI**
**MWANZA**
**MADAI TALAKA 77/2020**
**EDITHER PROSPER RWIKOZE**
**.......................................... MDAI**
**MASATU JACOBO .................... MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Mdai ameleta maombi ya kukaza hukumu dhidi yako hivyo unaamriwa kufika tarehe 12/03/2021 ili ueleze kwanini utekelezaji usifanyike.

**KUMBUKA KUWA:** Usipohudhuria siku hiyo ukazwaji wa Hukumu utafanyika na kuamuliwa bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya **Mahakama hii leo tarehe 23/02/2021**

**HAKIMU**
**MAHAKAMA YA MWANZO – MKUYUNI**
**MWANZA**

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**SHIJA EMMANUEL** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 963 CDT. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI: KAH/TR/RB/91//2021

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD &COURT BROKER**
**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE **30/03/2021** SAA NNE ASUBUHI TUTAUZA MAGARI AINA YA LANDCRUISER PRADO T 493 APS, MORANO T 979 DDJ, ISUZU FORWARD TIPPER T 493 AQR NA KIWANJA KILICHOPO NARA MALI YA JUMA SWAI BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA IMARISHA MAISHA LTD, S.L.P.4169 DODOMA. HIVYO TUNAPENDA KUWAKARIBISHA WAHITAJI WOTE.MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE (MAJANI YA CHAI).

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841.**


Tpb Bank
Grow with us

# PONGEZI



Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Benki ya TPB Plc inaungana na Watanzania wote kwa ujumla kumpongeza

**Mhe. Othuman Masoud Othuman Sharif**
Kwa kuteuliwa kuwa
Makamu wa kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

www.tpbbank.co.tz | info@tpbbank.co.tz, marketing@tpbbank.co.tz | facebook/tpbbank | 0787 669977


**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD &COURT BROKER**
**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 30/03/2021 SAA NNE ASUBUHI TUTAUZA GARI AINA YA TOYOTA IST T 559 DME NA KIWANJA KILICHOPO MTUMBA MALI YA EMMANUEL MZUNGU BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA IMARISHA MAISHA LTD, S.L.P.4169 DODOMA. HIVYO TUNAPENDA KUWAKARIBISHA WAHITAJI WOTE.MNADA HUO UTAFANYIKA MAENEO YA NYERERE SQUARE (MAJANI YA CHAI).

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841.**

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD &COURT BROKER**
**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 30/03/2021 SAA NNE ASUBUHI TUTAUZA GARI AINA YA TOYOTA CARINA T 183 CMV MALI YA BONIPHACE MWAKILEMBE BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA IMARISHA MAISHA LTD, S.L.P.4169 DODOMA. HIVYO TUNAPENDA KUWAKARIBISHA WAHITAJI WOTE.MNADA HUO UTAFANYIKA MAENEO YA NYERERE SQUARE (MAJANI YA CHAI).

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841.**


OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 -0782253676

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## HABARI KIMATAIFA

# Aung Suu Kyi 'atwishwa' kesi lukuki

**Yangon,** MYANMAR

KIONGOZI wa zamani wa Myanmar, Aung San Suu Kyi, aliyeondolewa katika mapinduzi ya kijeshi ya Februari Mosi, mwaka huu, ameshtakiwa jana, kwa makosa mawili mapya.

Hiyo ni kulingana na vyanzo kutoka timu yake ya mawakili.

Sasa anashtakiwa kwa kukiuka sheria ya mawasiliano ya simu na kuchochea machafuko, wakili Nay Tu alisema. Suu Kyi, anazuiliwa katika sehemu isiyojulikana mpaka sasa tangu kukamatwa kwake, alikuwa tayari ameshtakiwa kutofuata vizuizi vinavyohusiana na virusi vya corona.

Juzi, Ofisi ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa, ililaani ukandamizaji unaofanywa dhidi ya waandamanaji ikisema watu 18 waliuawa. Watu watano waliuawa katika mji wa Yangon chanzo kutoka Umoja wa Mataifa (UN), kimebaini.

Wakati huo Gazeti la Myanmar Now liliripoti kuwa watu wawili waliuawa katika mji wa pili wa Mandalay. Nchi mbalimbali zinaendelea kulaani ukandamizaji huo na ukatili vinavyoendeshwa na vikosi vya usalama, Myanmar. **RFI**

# Marekani yaandaa tamko mauaji Khashoggi

**Washington,** MAREKANI

MAREKANI imepanga kutoa tamko kuhusu Saudi Arabia baada ya ripoti yake ya kijasusi kusema kuwa, mrithi wa kiti cha ufalme wa taifa hilo, Mohammed Bin Salman aliamuru mauaji ya mwandishi wa habari, Jamal Khashoggi.

Rais wa Marekani, Joe Biden, mwishoni mwa wiki hii, alisema atatangaza wiki hii hatua watakayochukua kwa Saudi Arabia.

Utawala wa Biden umekosolewa hasa katika ripoti ya gazeti la Washington Post, iliyosema Biden angeonyesha nguvu zake kwa Mohammed Bin Salman, ambaye hakuwekewa vikwazo vya aina yoyote licha ya kutajwa kuhusika na mauaji ya Khashoggi.

Saudi Arabia ilifutilia mbali madai ya kumhusisha Mohammed Bin Salman na kifo cha Khashoggi, yaliyotolewa katika ripoti ya Marekani, kwamba, aliidhinisha mauaji ya Khashoggi mwaka 2018.

Kabla Saudi Arabia ilisema mauaji ya Khashoggi kwenye ubalozi mdogo wa Saudi Arabia nchini Uturuki, yalifanywa katika operesheni ya kihalifu na kukanusha kuhusika kwa mwanamfalme, Salman. **RFI**

# Gari la kifahari Bobi Wine kuchunguzwa

**Kampla,** UGANDA

**Bobi Wine, amekataa kuwasilisha gari hilo kwa misingi kwamba agizo hilo haliambatani na sheria.**

KIONGOZI wa upinzani Uganda, Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi Wine, yupo mashakani kwa madai ya kuwa na gari ambalo haliingii risasi, gazeti la Daily Monitor, ilisema.

Gari hilo limefanya mamlaka nchini humo na Mamlaka ya Ukusanyaji Ushuru ya Uganda (URA), ikisema maelezo yaliyotolewa si sahihi na kwamba thamani yake iko chini kuliko inavyostahili kuwa.

URA, sasa inataka gari hilo kukaguliwa upya.

Bobi Wine, amekataa kuwasilisha gari hilo kwa misingi kwamba agizo hilo haliambatani na sheria.

"Japo mna uwezo chini ya kifungu cha 236(d) cha usimamizi wa forodhani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki EAC, kukagua bidhaa, hamna uwezo wa moja kwa moja kukagua tena bidhaa ambayo ilikuwa katika (bohari yenu), na ambayo ilikuwa imekaguliwa, kutathmini kodi na kodi hiyo kulipwa kabla ya bidhaa kutolewa kwa mmiliki/mlipa kodi," ilisema.

Gari hilo liliingizwa nchini na kusajiliwa Kenya mwaka jana na kisha kupelekwa Uganda kupitia mpaka wa Busia. Katika ujumbe alioweka mtandaoni Februari 21, Kyagulanyi alidai kuwa gari hilo aina ya Toyota Land Cruiser, alipewa kama msaada na marafiki, wafuasi wake wa Uganda na ughaibuni. **BBC**



Siku ya kwanza ofisini katika makao makuu ya Shirika la Biashara Duniani (WTO), Mkurugenzi Mkuu mpya shirika hilo, Ngozi Okonjo-Iweala (katikati), akiwa na manaibu wakurugenzi wakuu wa shirika hilo, Alan Wolff (kushoto) na Karl Brauner, Geneva, Uswisi, jana. **Picha: AP**

# Huawei yaunga mkono mpango SDG's

**Shanghai,** CHINA

KAMPUNI ya Huawei imeunga mkono mpango wa Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (UN SDG's) katika kujenga dunia ya kijani.

Ilisema, ubunifu, umoja ikiwamo teknolojia inaweza kufanya kazi kama injini ya maendeleo ya binadamu.

Akizungumza katika mkutano wa masuala ya ushirikiano, ukuaji na ufanisi wa masuala ya teknolojia, uliofanyika Shanghai, Makamu wa Rais Mwandamizi wa Huawei na Mjumbe wa Bodi, Catherine Chen (pichani), alisema teknolojia inaweza kuwa injini ya maendeleo ya binadamu.

Pia alitoa wito kwa watu binafsi na wafanyabiashara kufikiria mambo makubwa zaidi.

Chen alisema ni muhimu kwamba watu wawe karibu zaidi na teknolojia ambayo ni nguzo sahihi ya kufikia malengo ya maendeleo.

"Mabadiliko makubwa ya kijamii huwa yanatokea na kuonekana kupitia mafanikio katika sayansi na teknolojia. Lakini leo, maendeleo ya kiteknolojia yanayoripotiwa ni ya kisiasa, kama wakati mwingine imekuwa hivyo kwa teknolojia 5G."

Chen alisema teknolojia hiyo ina upeo wa juu na muunganisho mpana, unaoweza kufaidisha wote na kwamba Afrika Kusini, Huawei, Shirika la Click Foundation waliungana na kuunganisha zaidi ya shule za msingi 100, mijini na vijijini kwenye huduma za intaneti, kuongeza ujuzi wa kusoma, kuziba pengo la kidigitali kupitia teknolojia.

Pia, nchini Kenya, Huawei ilishiriki katika kujenga Digitrucks, vyumba vya madarasa vinavyotumia umeme wa jua ambavyo huleta ustadi wa kidijiti kwa



jamii za pembezoni, ambazo hazina huduma hiyo.

Chen alisema teknolojia ya Smart PV katika nchi zaidi ya 60 imesaidia kufikia SDG's na kupunguza uzalishaji wa kaboni kiasi cha tani milioni 148.

"Hii ni sawa na kupanda miti zaidi ya milioni 200. Nchini Ethiopia pekee, tumesaidia wateja wetu kupeleka zaidi ya vituo 400 vya umeme wa jua, kupunguza uzalishaji wa kaboni kwa tani 2,850.

Nchini China, tumesaidia kujenga vituo vikubwa zaidi vya jua maalum kwa kilimo na uvuvi katika miji wa Ningxia na Shandong. "

Alisema, Huawei na UNESCO wameshirikiana imewezesha shule za Misri, Ethiopia, na Ghana kuboresha ujuzi wao wa kidijiti kupitia elimu ya mtandaoni.



# ALABA AGOMBEWA ULAYA

**ROME,** Italia

LIVERPOOL, Chelsea na Paris Saint-Germain zinajaribu kutaka kumsajili nyota anayetaka kuondoka, Bayern Munich, David Alaba, kwa mujibu wa mwandishi wa habari, Fabrizio Romano wa Sky Sport.

Alaba anaonekana kutaka kuondoka Bayern Munich na kujiunga na Real Madrid ya Hispania.

Nyota huyo wa kimataifa wa Austria, anataka changamoto mpya baada ya kukaa kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, akiwa amekaa na mabingwa hao Bayern kwa muda wa miaka 13.

Na kwa mujibu wa ripoti ya mwandishi huyo, miamba hiyo imekuwa kwenye mbio moja ya kumuwania Alaba.

Alaba ataondoka Bayern kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu huu baada ya mkataba wake kumalizika na mabingwa wa LaLiga, Real Madrid ndio wanaonekana wenye nafasi kubwa zaidi ya kumsajili.

Hata hivyo, Liverpool, Chelsea na PSG nazo zinaonekana zimekaza uzi kwenye kuwania saini ya nyota huyo.

# Guardiola afunguka kiwango cha Aguero

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola atamtumia Sergio Aguero kwa umakini, wakati akielezea ugumu wa kumpanga kila mchezaji kwenye kikosi cha Manchester City kilichojitosheleza.

City ilishinda mechi yake ya 20 mfululizo kwenye mashindano yote Jumamosi, wakati wakiichapa West Ham 2-1 kwenye Ligi Kuu, shukrani kwa mabao ya walinzi, Ruben Dias na John Stones.

Aguero alianza mechi yake ya nne msimu huu na ya kwanza tangu Oktoba mwaka jana, ambapo mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu wa 2020-21, huku akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, alishindwa kupiga shuti lolote langoni na alitengeneza nafasi moja tu na alitolewa nje dakika ya 61, akiwa amegusa mpira mara 32, ikiwa ni mara chache zaidi kuliko mchezaji yeyote aliyeanza kwa Man City katika mchezo huo.


Hata hivyo, Guardiola alisisitiza kuwa Aguero atatakiwa kurudisha kasi yake, ingawa dakika za kucheza za mshambuliaji huyo zitaangaliwa kwa makini.

"Sergio amekuwa nje kwa zaidi ya mwaka, alicheza, lakini aliumia na akafanyiwa operesheni," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa Sergio, hii ni sehemu ya msimu, ana kipaji cha ukweli na uwezo mkubwa wa kufunga mabao, hivyo akiwa fiti atatusaidia.

"Hivyo ni vizuri kwamba, alicheza kwa dakika 60, hilo ni jambo zuri kwa miguu yake. Kwenye mchezo unaofuata, pengine tutamhitaji kwa dakika 10, 15 au kuanzia mwanzo.

"Si jambo rahisi kwake, lakini anatakiwa kucheza katika ubora wake na ubora wa kutusaidia sisi."






# *AC Milan yapiga hesabu Tomori*

**MILAN,** Italia

MKURUGENZI wa Ufundi wa AC Milan, Paolo Maldini, amesema klabu hiyo inafikiria kumsajili, Fikayo Tomori kwa mkataba wa kudumu kutoka kwa miamba wa Ligi Kuu England, Chelsea.

Tomori amekuwa na kiwango cha kuvutia tangu atue hapo kwa mkopo Januari, na nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, amekuwa na mchango mkubwa kwa kikosi hicho, huku pia akichangia kwenye ushindi wa Milan wa 2-1 dhidi ya Roma, Jumapili.

Milan ina kipengele cha kumnunua Tomori mwishoni mwa msimu kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 25.

Alipoulizwa kuhusu majaliwa ya Tomori baada ya ushindi wa Milan kwa Roma ugenini, Maldini aliiambia Sky Sport Italia: "Tomori ana kipaji kizuri na tuna kipengele cha kumnunua moja kwa moja.

"Bei ni kubwa sana. AC Milan itaamua mwishoni mwa msimu na tutajadiliana na bodi ya Chelsea."

"Bahati mbaya, nafanya kazi kwenye klabu ambayo inawavutia wachezaji wengi. Wakati AC Milan ikiwaita wachezaji, wanasikiliza," aliongeza Maldini.

"Fikayo ni mchezaji mwenye sifa ya aina yake, kasi na akili nyingi akiwa uwanjani, hivyo nafikiri tunaweza kumsajili kwa ajili ya kuimarisha kikosi chetu."

# Bale: Nimekuwa na furaha msimu wote

**LONDON,** England

GARETH Bale amekanusha madai kwamba amekuwa katika wakati mgumu kwenye kipindi chake cha pili cha kucheza pale Tottenham Hotspur, akisisitiza "amekuwa na furaha msimu wote."

Bale alianza katika mchezo wake wa tatu wa Ligi Kuu msimu huu wa 2020-21 kwa staili ya aina yake, akifunga mara mbili na kutengeneza bao moja, wakati Spurs ikiifumua Burnley 4-0, Jumapili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alitua hapo kwa mkopo akitokea Real Madrid Septemba, alianza kufunga sekunde ya 68 likiwa bao la haraka zaidi Burnley kufungwa kwenye Ligi Kuu England.

Na Bale sasa amehusika kwenye mabao saba katika mechi nne zilizopita za Tottenham katika mashindano yote (mabao manne, pasi za mwisho tatu).

Raia huyo wa Wales hajawa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi tangu aliporudi tena hapo London, lakini kocha Jose Mourinho amekuwa akitaka kumtumia mara kwa mara kwenye ligi.

Mourinho alionekana kutoridhishwa wakati Bale alipoomba kuachwa kwenye kikosi cha Spurs kilichosafiri kwenda kucheza na Everton kwenye mchezo wa Kombe la FA, mapema mwezi uliopita kutokana na kuwa majeruhi.

Hata hivyo, Bale mwenyewe amebainisha kwamba, amekuwa na furaha kubwa tangu amerudi kwa mara ya pili kwenye kikosi hicho.

"Si jambo la kufunga mabao. Ni suala la wachezaji wote kuisaidia timu," alisema Bale akiiambia BBC Sport.

"Nimefurahi kufunga mabao na kutoa pasi za mwisho, lakini chochote ninachofanya nafanya kwa ajili ya timu.

"Nimekuwa na furaha msimu wote. Kwenye vyumba vya kubadilishia nguo nako niko poa na nafurahia."





# SOLSKJAER ALALAMIKIA WASHAMBULIAJI WAKE

**LONDON,** England

OLE Gunnar Solskjaer hakuficha hisia zake dhidi ya washambuliaji wa Manchester United baada ya kutoka sare ya bila kufungana na Chelsea Jumapili, kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Man United kwa mara nyingine ilishindwa kuondoka na ushindi kwenye mchezo dhidi ya timu sita za juu kwenye msimamo.

Mchezo huo ulimalizika kwa Man United kulalamikia kunyimwa penalti na mwamuzi, Stuart Attwell baada ya Callum Hudson-Odoi kuunawa mpira eneo la hatari.

Wakati Solskjaer na Luke Shaw walionekana kupaza sauti kwa hasira baada ya mwamuzi kutowapa penalti, kocha huyo alibadilisha upepo wakati akizungumza na waandishi wa habari na kuwageukia washambuliaji wake.

"Hatufungi mabao ya kutosha, hilo ni kwa uhakika kabisa," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Kabla ya mchezo huu niliwaambia wachezaji tunatakiwa kushinda, kupata mabao na kuondoka na pointi tatu.

# *Klopp sasa akunwa na ushindi akiihofia Chelsea*

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amedai Liverpool ilifanya kazi nzuri kupata ushindi dhidi ya Sheffield United, lakini anajua mchezo ujao wa Alhamisi dhidi ya Chelsea utakuwa changamoto ngumu.

Liverpool ilimaliza ukame wa kutoshinda mechi nne za ligi baada ya kushinda 2-0 pale kwenye dimba la Bramall Lane.

Curtis Jones alianza kufunga bao la kwanza na la pili kwake kwenye ligi, kabla ya Roberto Firmino kufunga la pili.

Oli McBurnie na Oliver Burke wote walikosa nafasi ya kusawazisha kwa Sheffield. Liverpool sasa inajiandaa na mchezo ujao dhidi ya kikosi cha Thomas Tuchel, Chelsea utakaopigwa pale Anfield.

Tuchel ambaye alimrithi Klopp kule Borussia Dortmund kabla ya kwenda kuinoa Paris Saint-Germain na sasa 'Blues' hao, Jumapili alitoka sare ya bila kufungana na Manchester United.

Ushindi utawafanya Liverpool kupanda juu ya Chelsea, ingawa kama wakifungwa itawafanya kufifisha matumaini ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu.

"Ni muhimu sana. Watu wengi walishapoteza matumaini kwa upande wetu. Ushindi huu ni muhimu kwetu," alisema Klopp akiiambia Sky Sports.

"Usiku huu (juzi) tulionyesha kwamba, bado tupo imara, lakini Alhamisi tutacheza na Chelsea na tunatakiwa kushinda tena.

"Lakini matatizo makubwa tuliyo nayo bado yanatuzunguka. Tunatakiwa kuyamaliza na kuwa kwenye nafasi nzuri."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI ULAYA



# TUCHEL AMSHANGAA REFA KUINYIMA UNITED PENALTI

●●● Kwa upande wangu ilikuwa ni penalti, ilinishangaza na bado nashangaa, marudio yalionyesha...

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amesema "alishangazwa" na uamuzi wa kutopewa penalti Manchester United kwenye mchezo wao wa sare wa Ligi Kuu ya England juzi, Jumapili.

**United waliachwa na hasira baada ya kukataliwa kupewa penalti kipindi cha kwanza kwenye mchezo huo uliopigwa pale kwenye dimba la Stamford Bridge.**

Katika kipindi hicho cha kwanza, mwamuzi, Stuart Attwell, aliangalia kama anatakiwa kuwapa penalti United wakati mpira ulipomgonga kwenye mkono Callum Hudson-Odoi, ambaye alikuwa akikabana na Mason Greenwood.

Attwell akaamua kuachana na uamuzi wa kutoa penalti na kitendo hicho kiliamsha hasira kwa kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer na mlinzi wa pembeni, Luke Shaw.

Baada ya mchezo, Tuchel ambaye ni kocha wa pili kwa kikosi chake kutoruhusu nyavu zake kutikiswa katika mechi nne mfululizo za Ligi Kuu nyumbani baada ya Brendan Rodgers wakati akiinoa Swansea City msimu wa 2011-12 - aliwaambia waandishi wa habari: "Kwa upande wangu ilikuwa ni penalti. Ilinishangaza na bado nashangaa.

"Sikuona mwanzo, lakini marudio yalionyesha kuwa Manchester United walitakiwa kupewa penalti. Hadi sasa sijui kwa nini haikuwa penalti."

Ulikuwa mchezo mwingine wa sare kati ya Chelsea na United mechi zote zikiwa za ligi wakishindwa kufungana mabao kwa mara ya pili baada ya msimu wa 1921-22.

Chelsea haijafungwa tangu Tuchel achukue nafasi ya kocha, Frank Lampard na mechi 10 bila kufungwa katika mashindano yote.

Tuchel na Chelsea yake wanashika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu, pointi moja wakipitwa kutoka kwenye nne bora, sita nyuma ya wanaoshika nafasi ya pili, United na wakipitwa 18 na vinara Manchester City baada ya kushuka dimbani mara 26.

"Tulitakiwa kuwa na matokeo makubwa. Tulijaribu kwa kila kitu kuhakikisha tunashinda, lakini tukamaliza kwa sare na tupo katikati ya kupambania kuingia kwenye nne bora."

## ZISIKUPITE

### MESSI, RONALDO WATAKIWA

MMILIKI mwenza wa Klabu ya Inter Miami, David Beckham, amesema anataka kuwasajili nyota wa Argentina na Barcelona, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33 na mkali wa Ureno na Juventus, Cristiano Ronaldo, 36, wakacheze katika klabu hiyo ya Ligi Kuu Marekani, MLS. ***(Mirror)***

### ARTETA ATAJWA BARCELONA

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta yupo kwenye orodha ya mgombea urais wa Barcelona, Joan Laporta kuchukua nafasi pale Nou Camp. ***(Mirror)***

### BAYERN YAMWANIA KOULIBALY

BAYERN Munich imetoa ofa ya euro milioni 45 kwa mlinzi wa kati wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly, 29. ***(Tuttomercatoweb, via Caught Offside)***

### TOMORI ATAKIWA JUMLA MILAN

MKURUGENZI wa Ufundi wa AC Milan, Paolo Maldini, anataka kufanya mazungumzo na Chelsea kuhusu ada ya pauni milioni 26 ya usajili wa kudumu wa mlinzi wa kati wa England, Fikayo Tomori, 23, anayecheza kwa mkopo kwa miamba hao wa Serie A. ***(Sky Sports)***

### LOCATELLI AGOMBEWA ULAYA

REAL Madrid imeingia kwenye mbio moja na Manchester City na Juventus kuwania kumsajili kiungo wa Sassuolo na Italia, Manuel Locatelli, 23. ***(Calciomercato)***

### LAMBERT KUINOA CELTIC

PAUL Lambert anaweza kuchukua nafasi ya kuwa kocha wa Celtic baada ya kuachia nafasi yake kule Ipswich Town. ***(Scotsman)***

### SALAH MCHEZAJI MUHIMU LIVER

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema straika Mmisr, Mohamed Salah "ni mchezaji muhimu sana" kwa klabu hiyo na ana matumaini nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 "atakuwa hivyo kwa muda mrefu." ***(Liverpool Echo)***

### TAVARES AWINDWA EPL

BURNLEY na Newcastle United zinamfuatilia kwa karibu mlinzi wa Ureno, Nuno Tavares, 21, huku timu ya Napoli ya Italia pia ikionyesha nia ya kumtaka mchezaji huyo wa Benfica. ***(O Jogo)***

### ANCELOTTI NA USAJILI EVERTON

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti, amesema walimsajili kiungo Abdoulaye Doucoure, 28, kutoka Watford kwa baraka za Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, Marcel Brands. ***(Liverpool Echo)***

### RHODES AWANIWA CARDIFF

KOCHA wa Cardiff City, Mick McCarthy, anawania kumsajili straika wa Scotland, Jordan Rhodes, 31, kipindi cha majira ya joto kinachokuja, wakati mkataba wa mchezaji huyo utakapomalizika kule Sheffield Wednesday. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

## Simba yatoa sababu kumrejesha Rweyemamu

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba ambayo imeamua kumrejesha meneja wake wa zamani, Patrick Rweyemamu, kuendelea na nafasi yake hiyo, imefunguka kuwa haijawahi kutamka au kumtuhumu kuhujumu timu yao.

Akizungumza Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Klabu ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again', alisema hakuna kiongozi yeyote wa klabu hiyo aliwahi kusema kuwa meneja wao Rweyemamu amehujumu timu.

"Klabu haijawahi kusema amesimamishwa kwa ajili ya kuhujumu timu, wala hakuna kiongozi yeyote ambaye aliwahi kutamka hivyo," alisema Try Again.

Alisema ni kweli wamemrudisha meneja huyo baada ya kufanya uchunguzi na kujiridhisha kuwa kila kitu kipo sawa na sababu za msingi ambazo walimwondoa sasa hazipo tena, hivyo wameamua kumrejesha kwenye nafasi yake.

Alisema wanaimani kubwa na meneja huyo kwa sababu wamefanya naye kazi kwa miaka mingi ndani ya klabu hiyo tangu akiwa kwenye timu ya vijana U-20.

"Amefanya kazi Simba kwa miaka mingi tangu akiwa na timu ya vijana na sasa anarudi kundini, hivyo Wanasimba wote tunatakiwa tuendelee kumpa sapoti," alisisitiza.

## ZFF: Hukuna kushuka daraja ligi zote Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF) limesema katika msimu huu wa 2020/ 2021 hakuna timu itakayoshuka daraja kwa ngazi zote za ligi visiwani hapa.

Hayo yameelezwa jana na Kaimu Katibu Mkuu wa ZFF, Haji Hasssan "Kibabu", ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa wa Mjini Magharibi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika Ukumbi wa Mikutano wa shirikisho hilo.

Alisema uamuzi huo umekuja baada ya Kamati ya Utendaji ya ZFF kukutana kwa dharura Kisiwani Pemba kujadili mambo mbalimbali ikiwamo mwenendo mzima wa ligi katika msimu huu pamoja na hali ya kujiuzulu kwa aliyekuwa Rais wa Shirikisho hilo, Seif Kombo Pandu pamoja na Mkurugenzi wa Mashindano, Ali Mohmmed Ameir.

Alisema kamati hiyo imekubaliana kufanya marekebisho ya kanuni ya mashindano ya msimu huu wa 2020/2021 ikiwamo katika suala la kushuka daraja ambapo msimu huu timu hazitashuka kwa ngazi zote kwa Kanda ya Pemba na Unguja.

# MSUVA AIFIKISHA WYDAD MATAWI YA SIMBA CAF

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Simon Msuva, ametoa mchango mkubwa kwa klabu yake ya Wydad Athletic Club (Wydad Casablanca) kwa kuiwezesha kufikisha pointi sita kama ilivyo kwa Simba kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi baada ya juzi kuifungia bao moja katika ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Kaizer Chiefs FC ya Afrika Kusini.

Ushindi huo unaifanya Wydad Casablanca ambayo ipo Kundi C pamoja na Horoya FC, Kaizer Chiefs na Petro de Luanda, kuungana na Simba na Mamelodi Sundowns kutoka Kundi A na B, kuwa timu pekee hadi sasa zilizoshinda mechi zake mbili za mwanzo na kuongoza makundi yao.

Simba ipo Kundi A pamoja na Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh ya Sudan, wakati Mamelodi Sundowns ikiwa Kundi B pamoja na TP Mazembe, Al Hilal na CR Belouizdad.

**Katika mchezo huo wa Kundi C uliopigwa Uwanja wa Du 4 Aout jijini Ouagadougou nchini Burkina Faso, Wydad ndiyo ilikuwa wenyeji wa Kaizer Chiefs kutokana kuwapo kwa sheria kali ya watu kutoka Afrika Kusini kuingia Morocco kwa sababu ya COVID-19, hivyo Wamorocco hao kuamua mechi yao ya nyumbani ichezewe Burkina Faso.**

Kwenye ushindi huo Msuva alifunga bao la tatu dakika ya 86 akimalizia pasi ya Walid El Karti huku mabao mengine ya Wydad yakifungwa na Mohammed Ounajem dakika ya saba, Ayoub El Kaabi dakika ya 44 na Yahya Jabrane ambaye alifunga kwa penalti dakika ya 90.

Kwa ushindi huo, Wydad inafikisha pointi sita katika Kundi C ikifuatiwa na Horoya ya Guinea yenye ponti nne, Kaizer Chiefs pointi moja na Petro de Luanda ya Angola ikiburuza mkia baada ya kupoteza mechi zote mbili za kwanza.

Katika mechi nyingine ya Ligi ya Mabingwa iliyopigwa juzi, Mamelodi Sundowns nayo ilifikisha pointi sita, tatu kati ya hizo ikizivuna katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kwa kuichapa CR Belouizdad ya Algeria kwa mabao 5-1.

CR Belouizdad ndiyo ilikuwa mwenyeji baada ya kuomba mechi hiyo ipigwe Tanzania kutokana na sheria kali nchini Algeria dhidi ya watu kutoka Afrika Kusini, kutokana na kuhofia maambukizo mapya ya virusi vya corona.

WAKUOGELEA...




Mabingwa wa kuogelea wa mashindano ya Taliss, Klabu ya Bluefins, wakiwa na medali zao baada ya kukabidhiwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# *Bluefins mabingwa wa kuogelea Taliss*

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya kuogelea ya Bluefins, imetwaa ubingwa wa mashindano ya Taliss baada ya kukusanya pointi 1,619 na kuzidi klabu nyingine tano zilizoshiriki michuano hiyo iliyofanyika kwenye bwawa la kuogelea la Klabu ya Gymkhana jijini Dar es Salaam.

Kati ya pointi hizo, 872 zilipatikana kwa upande wa wanaume na 747 kwa wanawake. Klabu ya Dar es Salaam Swimming illishinda nafasi ya pili kwa kupata jumla ya pointi 1,592 na waandaaji wa mashindano hayo, Taliss walishinda nafasi ya tatu kwa kupata pointi 1,308.

Klabu ya Mwanza (MSC) ilimaliza katika nafasi ya nne kwa kupata pointi 954 na FK Blue Marlins ikishika nafasi ya tano kwa kupata pointi 854. Timu ya Morogoro (Mis Piranhas) ilishika nafasi ya sita baada ya kujikusanyia pointi 595.

Katika mashindano hayo, klabu ya Bluefins ilishinda jumla ya medali 52 ambapo kati ya hizo, 24 ni dhahabu, 11 fedha na 17 shaba. Muogeleaji mwenye umri wa miaka 10, Maryam Ipilinga alivuna pointi nyingi zaidi kwa klabu hiyo kwa kujikusanyia pointi 115 baada ya kushinda medali tano za dhahabu.

Muogeleaji huyo alifuatiwa na Aminaz Kachra (11) aliyevuna pointi 109 kwa kushinda medali tatu za dhababu na mbili za fedha huku Lina Goyayi (11) alivuna pointi 100 kwa kushinda medali mbili za dhahabu na moja ya shaba.

Michezo
Jumanne Machi 2, 2021
Nipashe



Tuchel amshangaa refa kuinyima United penalti UKURASA 22

PENALTI AISEE...



Winga wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi (kulia), akionekana kuunawa mpira ndani ya eneo lao la hatari, suala ambalo beki wa Manchester United, Luke Shaw na kocha wa kikosi hicho, Ole Gunnar Solskjaer baada ya mchezo huo wa Ligi Kuu England uliopigwa Uwanja wa Stamford Bridge juzi, walimtupia lawama mwamuzi Stuart Attwell kwa kuwanyima penalti. **HABARI UK. 21**

# KAZE ATAJA DAWA YA 3 ZA COASTAL YANGA

## ●●● Akiri Carlinhos kumtibulia hesabu za mwanzo huku uongozi ukija na mkakati kukarabati jengo wakati...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

LICHA ya kukiri kuwa kukosekana kwa kiungo Carlos Carlinhos, kwenye kikosi chake ni pengo kwa sababu tayari alikuwa ameshaanza kuchanganya na kufanya vema baada ya kuanza kucheza akitoka kwenye chumba cha majeruhi, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, ametaja mbinu zinazoweza kumpa matokeo chanya na kuibuka na pointi tatu dhidi ya Coastal Union.

**Yanga inatarajia kucheza mechi yake ya Ligi Kuu Alhamisi katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga dhidi ya Coastal Union na itamkosa Muangola huyo ambaye alilimwa kadi nyekundu Jumamosi wakati timu hiyo ikicheza Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam dhidi ya Ken Gold ya Mbeya kwenye Kombe la FA.**

Kaze alisema Carlinhos aliingia kirahisi kwenye mtego ambao alishinda kuutambua, hivyo kujikuta akifanya kosa ambalo hakulitarajia.

"Tukio halikuwa kubwa kivile, lakini mwenyewe alishindwa kujidhibiti na kujikuta akiingia kwenye mtego kirahisi. Ni pengo kwa timu kwa sababu kwenye mechi chache ambazo amecheza tangu atoke majeruhi, ameonyesha kuwa ana msaada mkubwa kwa wenzake," alisema Kaze.

Mchezaji huyo ndiye aliyefunga bao pekee Februari 20 kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Mtibwa Sugar, akitokea benchi, ikiwa ni mechi yake ya kwanza, baada ya kukaa nje kwa muda mrefu akiwa majeruhi.

Hata hivyo, Kaze alisema anachoshukuru ameomba radhi na mambo yamekwisha, lakini wao wanakwenda kucheza mechi zinazofuata na wachezaji waliopo.

Kuhusu mechi dhidi ya Coastal Union, Kaze alisema kubadilisha mbinu ni kitu muhimu kwake katika mchezo huo ili kuweza kupata alama tatu.

Kaze aliliambia Nipashe kuwa mpango mkubwa ni kupata matokeo chanya kwenye mechi yao ijayo dhidi ya Coastal Union na tayari amefanyia kazi kasoro zilizojitokeza katika kikosi chake na sasa wachezaji wake wapo vizuri, hivyo anaamini atapata matokeo chanya na kuzidi kujiimarisha kileleni.

"Kwa sasa tunatazama namna gani tunaweza kupata matokeo chanya kwenye mechi zijazo, hilo ni la msingi kwetu, katika hilo ni kuendelea kuwapa mbinu washambuliaji ili kuweza kumalizia nafasi wanazotengeneza uwanjani," alisema Kaze.

Alisema wamekuwa wakitengeneza nafasi zaidi ya tano na kushindwa kumalizia jambo ambalo amekuwa nalo makini kwa washambuliaji wake katika mazoezi.

"Kila kitu kitakuwa sawa mashabiki waendelee kutupa sapoti kwa kuwa ushindani ni mkubwa nasi pia tunaendelea kushindana, kuhakikisha tunapata pointi tatu muhimu katika mchezo huo," alisema Kaze.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla amesema kwa sasa wanafanya ukarabati vyumba vya jengo ambapo chumba kimoja kitagharimu shilingi milioni sita

"Tumeshaanza kufanya ukarabati huo kwa chumba kimoja na kuna vyumba 30 ambavyo vinatakiwa kufanyia ukarabati huo," alisema Msolla huku akifafanua kuwa tayari baadhi ya wanachama wametoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa vyumba saba.

# Onyango atangaza kuja kizee Simba SC

**Na Adam Fungamwango**

BEKI kisiki wa Simba, Mkenya Joash Onyango, amesema anakaribia kuweka tena rangi nyeupe kwenye ndevu zake ili zionekane ana mvi mithili ya mzee kama alivyowahi kufanya akiwa nchini Kenya.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Onyango alisema baada ya mechi tatu au nne, ataweka tena rangi nyeupe ndevu zake kwa ajili ya kuwatumia salamu wajukuu zake.



Onyango alifafanua kuwa wajukuu zake ni wale waliokuwa wakimbeza kuwa yeye ni mzee na klabu ya Simba imesajili mchezaji mwenye umri mkubwa.

"Nakaribia kuzirudisha tena ndevu zangu nyeupe, sasa niwe babu kabisa kwa wajukuu zangu, niwatumie salamu," alisema Onyango.

Kabla ya kujiunga na Simba, Onyango alikuwa gumzo akiwa kwenye kikosi cha Harambee Stars ya Kenya, alipoamua kupaka rangi nyeupe ndevu zake na kuonekana kama mzee, na hata alipojiunga na Klabu ya Simba, picha zake hizo zilitumika na mashabiki wengi wakibeza usajili wake.

Wakati Onyango akitaka kurudisha mvi zake, tayari mashabiki wa Tanzania wameshabadilisha mtazamo na kumchukulia kuwa ni mmoja wa mabeki bora kabisa nchini kwa sasa.

Kuhusu hali ya usajili wake kubezwa, Onyango alisema kuwa hawezi kumlaumu mtu yoyote kwani kila mtu ana mtazamo wake.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >